Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 13, NOVEMBA 2023

TUNABORESHA AFYA
MTU NI AFYA • AFYA NI MTAJI

## MUSWADA WA BIMA YA AFYA KWA WOTE WAPITA KWA KISHINDO



BIMA YA AFYA KWA WOTE
UHAKIKA WA MATIBABU KABLA YA KUUGUA

# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO




## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. John Jingu
KATIBU MKUU

**MHARIRI**
Englibert Kayombo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Emmanuel Malegi

**WAJUMBE**
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Majid Abdulkarim
Said Nyaoza
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga

**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz

# YALIYOMO

Muswada wa sheria ya bima ya afya kwa wote wapita kwa kishindo...UK 1





Rais samia atoa shil. Bilioni 9 kusomesha wataalamu bingwa na bobezi wa afya 601.... UK 2

Kifo cha mariam chanzo ni wahudumu wa afya sio kukosa fedha.... UK 3





Serikali kukamilisha ujenzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa wa songwe kwa wakati..... UK 4

Wataalamu wa afya watakiwa kuzingatia mafunzo ya chati uchungu kupunguza vifo vya mama na mtoto.... UK 5





Mpango mpya wa kutokomeza vvu, magonjwa ya ngono na homa ya ini wazinduliwa.... UK 7

Serikali kuendelea kuimarisha upatikanaji wa rasilimali watu katika sekta ya afya.... UK 8



Wahandisi wa vifaa tiba na wataalamu wa afya tunzeni vifaa kwa maendeleo ya sekta ya afya .... UK 9





Waziri Ummy akabidhi vifaa vyenye thamani ya tsh: mil. 156 kwa waraibu Tanga .... UK 10

Waganga wakuu wa mikoa na wilaya jumuisheni afua za kifua kikuu na ukoma wakati wa afua nyingine .... UK 12





Waganga wakuu wa mikoa na halmashauri simamieni huduma za matibabu ya meno kabla ya kufikia kung'oa... UK 13

"Tuunge mkono kwa vitendo jitihada za dkt. Samia katika sekta ya afya ", dkt. Mollel .... UK 16





Viongozi wa hospitali na timu za afya simamieni ubora wa huduma za afya kwa wananchi .... UK 17

Viongozi wa sekta ya afya simamieni ubora wa huduma za afya nchini.... 18





Matumizi ya vyoo bora yameongezeka nchini tanzania.... UK 19



Onyo kwa wafamasia wanaouza dawa bila cheti cha daktar .... UK 20

Acheni kufanya kazi kwa mazoea, tunataka ubora wa huduma kwa wananchi", dkt mollel .... UK 21





70% ya magonjwa ya binadamu yanatokana na wanyama .... UK 22

Wataalam, wasimamizi na watoa hudumaza afya zingatieni viapo vya taaluma na weledi..... UK 23





Rais kikwete aipongeza serikali kwa juhudi za kupunguza vifo vya akinamama wajawazito .... UK 24

Dkt. Jingu akoshwa na huduma zinazotolewa hospitali ya mkoa morogoro.... UK 25





Hadubini 133 zakabidhiwa kwa ajili ya vyuo vya afya vya kati na vituo vya tafiti za magonjwa ya binadamu.... UK 26



# Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote wapita kwa kishindo

**Na. Emmanuel Malegi, Dodoma**

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaloongozwa na Mhe. Spika Dkt. Tulia Akson limepitisha muswada wa sheria ya bima ya afya kwa wote ya mwaka 2022.

Muswada huo wa sheria ya bima ya afya kwa wote ulipitishwa Novemba 01, 2023 baada ya kukwama mwezi Februari 2023 kwa kukosa vyanzo endelevu vya mapato.


Aidha Mhe. Spika Dkt. Tulia Akson alimpongeza Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu na Naibu Waziri Dkt. Godwin Mollel Pamoja na watendaji chini ya wizara ya afya kwa juhudi kubwa wanazozifanya katika sekta ya afya.

Hata hivyo Dkt. Tulia aliipongeza Kamati ya kudumu ya bunge ya Afya na masuala ya Ukimwi chini ya Mhe. Stanslaus Nyongo kwa juhudi kubwa za kufanikisha na kushirikiana na wizara katika kufikia lengo la muswada wa sheria ya bima ya afya kwa wote

Kwa upande wake Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema kutokana na upekee wa Bima ya Afya kwa Wote, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha wamependekeza baadhi ya vyanzo vya mapato ili kuendesha mfuko huo.

Vyanzo hivyo ni pamoja na sehemu ya mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vyenye kaboni, vinywaji vikali, bidhaa za vipodozi, kodi ya michezo ya kubahatisha, ada ya Bima za vyombo vya moto na mapato yatokanayo na ushuru wa miamala ya kielektroniki kwa kadiri itakavyopendekezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, fedha zitakazotengwa na Bunge, mapato yatokanayo na uwekezaji wa mfuko na zawadi pamoja na misaada kutoka kwa wadau mbalimbali.

Waziri Ummy aliyasema hayo Bungeni jijini Dodoma wakati akiwasilisha Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote ambao ulikwama mwezi Februari mwaka huu kwa hoja iliyotolewa na Bunge ya kutokuwepo kwa chanzo endelevu cha fedha za kutekeleza mpango huo.





# Rais Samia atoa shil. Bilioni 9 kusomesha Wataalamu bingwa na bobezi wa afya 601

**Na Hassan Kimweri,**
**Dar Es Salaam**

Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 9 kwa ajili ya kusomesha wataalam bingwa na bobezi 601 fani mbalimbali za afya ili kuongeza idadi ya wataalam wenye ujuzi wa kutoa huduma za kibingwa hapa nchini.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu Novemba 29, 2023 wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Mpango wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuongeza wataalam bingwa na bobezi wa afya nchini kwa mwaka wa fedha 2023/24.

"Tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 9 kwa ajili ya mafunzo ya wataalamu bingwa na bobezi katika fani mbalimbali za Sekta ya Afya ambapo fedha hizo ni muendelelezo wa uwekezaji mkubwa unaofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan." Amesema Waziri Ummy Mwalimu.

Waziri Ummy amesema fedha hizo zitatumika kugharamia mafunzo kwa wataalamu wapya 601 sawa na 92% ya waombaji ambao walikidhi vigezo vya kusomea utaalamu wa ubingwa na bobezi wa fani mbalimbali za Sekta ya Afya.

"Ufadhili huu ni kwa ajili ya kulipiwa ada ya mafunzo na posho ya utafiti kwa watakaofadhiliwa ndani ya nchi na kwa wanaoenda kusoma vyuo vya nje ya nchi watalipiwa ada, posho ya kujikimu wakiwa masomoni (Stipend), nauli ya kwenda na kurudi pamoja na posho ya utafiti." Amesema Waziri Ummy.

Aidha, Waziri Ummy amewataka wataalamu wote waliopata ufadhili huu wa mwaka 2023/2024 kukamilisha taratibu za kujaza mikataba ya ufadhili kama ishara ya kukubali ufadhili huu.
Amesema kuwa muda wa kujaza mikataba ya ufadhili ni kuanzia tarehe 29 Novemba, 2023 hadi 12 Disemba, 2023 na nakala ya mikataba hiyo inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Afya na pia itatumwa kwa barua pepe kwenye anuani za barua walizotumia wakati wa kuwasilisha maombi.



# Kifo cha mariam chanzo ni wahudumu wa afya sio kukosa fedha

**Na. Hassan Kimweri,**
**Tanga**

Tume iliyoundwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu kuchunguza kifo Cha mjamzito, Mariam Zahoro imebaini kuwa kifo hicho kilitokana na uzembe wa wataalam wa Afya na sio sababu ya kukosa fedha za kugharamia matibabu yake kiasi cha Tsh: 150,000.

Waziri Ummy alisema hayo baada ya kupokea taarifa kutoka kwa tume ya Uchunguzi aliyoiunda ikiongozwa na Dkt. Ally Said ambae ni Daktari bingwa na Mhandiri wa Magonjwa ya Akina Mama na Uzazi kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

"Kifo cha Mariam Zahoro kilitokea tarehe 11 Novemba, 2023 katika kituo cha Afya cha Kabuku baada ya kushindwa kujifungua kwa njia ya kawaida na hivyo kuhitaji kufanyiwa huduma ya dharura ya upasuaji ambapo huduma hiyo hakupatiwa kwa wakati na hivyo kupelekea kupoteza maisha." Alisema Waziri Ummy

Alisema, kifo hicho kimetokea kwa sababu ya Mtaalamu wa huduma ya Usingizi na ganzi kutopatikana licha ya kupigiwa simu mara kadhaa kuwa kuna dharura pamoja na Daktari wa zamu namba 2 kuchelewa kufika licha ya kupigiwa simu mara nyingi kuwa kuna dharura.

Daktari huyo namba 2 xxx hata alipofika hakuchukua hatua za kuokoa maisha ya mgonjwa kama kumpa rufaa baada ya mtaalamu wa usingizi kutopatikana au kutuma mtu wa kwenda kumgongea mtaalam wa huduma za usingizi." alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alisema Nchi yetu inaongozwa na Sheria na taratibu hivyo amelitaka Baraza la Madaktari Tanzania pamoja na Baraza la Wauguzi ambao wamepelekewa taarifa za Madaktari hao kuharakisha Mchakato wa Kusikiliza mashauri baada ya kukamilika kwa muda wa siku 14 baada ya wao kujieleza huku akisisitiza watumishi hao kutorudi kazini.

Pia, Waziri Ummy alipiga Marufuku kwa Viongozi na wataalamu kufanya maamuzi ya kuwatoza fedha wananchi kupitia vikao vya makubaliano pasi na kuwashirikisha wananchi kutokana na Majibu ya taarifa ya Uchunguzi kuonyesha kuwa yaliweka makubaliano ya kuwatoza wajawazito gharama hizo za Shilingi laki na nusu kwa watakojifungua kwa Upasuaji.





# Serikali kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Songwe kwa wakati

**Na Said Nyaoza,**
**Songwe**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imepanga kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe iliyopo katika kata ya Vwawa, Wilaya ya Mbozi mkoani humo kabla ya mwaka 2025

Hayo yalisemwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akizungumza na wananchi Hospitalini hapo katika ziara yake ya kuweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa Hospitali hiyo.

Mhe. Majaliwa alisema Rais wetu Mhe, Dkt. Samia Suluhu Hassan ataendelea kuleta fedha za kutosha mkoani Songwe ili kuhakikisha ujenzi wa Hospitali hiyo unakamilika kwa wakati.



"Ujenzi unaendelea na mpaka sasa Serikali imetumia shilingi bilioni 13 katika ujenzi wa majengo yaliyopo hapa na tunatarajiwa kutumia shilingi Bilioni 37 mpaka kukamilika kwake". Alisema.

Pia Mhe. Majaliwa alisema kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali hiyo ita imarisha huduma za Tiba utalii nchini kwa kuhudumia wagonjwa mbalimbali kutoka nchi za jirani.

"Hospitali hii inayojengwa hapa Songwe ni ya kimkakati, mkoa huu unapakana na nchi za jirani za zambia na malawi ndugu zetu kwahiyo ndugu zetu wa jirani wa karibu watakuwa wakina hapa mbozi kutibiwa". Alisema.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Afya Mhe. Dkt. Godwin Mollel alisema vifaa Tiba muhimu vyote vya kuweka katika Hospitali hyo vipo tayari kwa kufungwa ikiwemo kifaa cha CT Scan ambacho ndani ya siku 21 kitakuwa tayari kimeshafungwa Hospitalini hapo.

"Ndani ya hospitali hii kuna majengo yanamaliziwa lakini vifaa tiba vyote vipo hapa na vingine vipo kanda kwa ajili ya kuweka kwenye majengo ambayo yamemalizika, watu watakuwa hawana haja ya kusafiri zaidi ya kilometa 100 kwenda mbeya kufuata huduma za vifaa hivyo". Alisema Dkt. Mollel.

# Wataalamu wa afya watakiwa kuzingatia mafunzo ya chati uchungu kupunguza vifo vya mama na mtoto

**Na. Englibert Kayombo**
**Shinyanga**

Wataalamu wa Afya wametakiwa kutumia taaluma na ueledi walionao kwa kuzingatia mafunzo ya chati uchungu ili kupunguza idadi ya vifo vya Mama na Mtoto ambavyo vimekuwa vikijitokeza.

Hayo yalisema na Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Daniel Mzee, wakati akizungumza na Madaktari pamoja na Wauguzi Wakunga katika mafunzo ya Chati Uchungu yanayofadhiliwa na USAID kupitia mradi wa Afya Yangu yanayoendelea Mkoani Shinyanga.

Dkt. Mzee aliwaeleza wataalamu hao kuwa mafunzo hayo yana umuhimu mkubwa katika kuboresha Afya ya Mama na Mtoto, hivyo na ili kufanyika vizuri hawana budi kuyazingatia kwa kuyafanyia kazi kwa makini.

“Tusikilize vizuri mafunzo na tuzingatie miongozo kwa lengo la kupunguza vifo vya mama na motto, Bado kasi haijawa ya kuridhisha, lakini hapa tulipofikia ni pazuri hivyo tuendelee kupambana, Nina uhakika mtakapoenda kwenye maeneo yenu ya kazi mtatumia mafunzo haya kuwafundisha na wenzenu ili mboreshe huduma nzuri hususani katika kuokoa maisha ya mama na mtoto”, alisema Dkt. Mzee.

Kwa upande wake Mkunga Mbobezi kutoka Idara ya Huduma za Uuguzi na Ukunga Wizara ya Afya, Aziza Machanje, alisema Serikali imeelekeza kutolewa kwa mafunzo ya Chati Uchungu ambayo imeboreshwa zaidi kuzidi kukabiliana na changamoto zitokanazo na uzazi hasa kwa mama na mtoto.

“Chati Uchungu ni chati inayotumia kuangalia maendeleo ya mama mjamzito wakati wa kujifungua ili kujua maendeleo ya mama na mtoto tumboni, Tumeona umuhimu mkubwa wa kuwa nayo moja ili itumike nchini kote, na ndiyo maana Wizara imeamua kuandaa haya mafunzo kwa wataalamu wetu wa Afya”, alisema Machanje.



# Watumishi wawili wakutwa na tuhuma za kujibu kwenye kituo cha afya kabuku



**Na Englibert Kayombo**
**Tanga**

Watumishi wawili wakutwa na tuhuma za kujibu kwenye kifo cha Bi. Mariam Zahoro mkazi wa Kijiji cha Mumbwi katika Wilaya ya Handeni kilichotokea kwenye Kituo cha Afya Kabuku, Mkoa wa Tanga.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema hayo baada ya kupokea taarifa ya uchunguzi wa kifo cha mama mjamzito na kichanga chake katika kituo cha Afya Kabuku Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Mkoani Tanga.

"Serikali imepokea mapendekezo ya kamati iliyoundwa na tayari tumeanza kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT) kutoa notisi ya kumtaka Daktari kujibu tuhuma zinazomkabili - pamoja na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) kutoa notisi kwa Muuguzi na kutakiwa kujibu tuhuma hizi ndani ya siku 14 kuanzia leo." Alisema Waziri Ummy

Waziri Ummy wakati akifafanua taarifa hiyo alisema kuwa Watumishi hao wawili ambao ni Daktari wa zamu namba 2 (Dkt xxx) na Muuguzi wa kutoa huduma za usingizi xxx kushindwa kuzingatia maadili na weledi wa taaluma zao katika kumuhudumia mgonnjwa huyu.

"Kamati imebaini kuwa Daktari wa zamu namba 2 alishindwa kufika kwa wakati kutoa huduma za dharura licha ya kupewa taarifa mara kwa mara ya kutakiwa kufika Kituoni kutoa huduma ya dharura kwa mgonjwa huyu." Alisema Waziri Ummy

Alisema, Daktari huyu licha ya kufika Kituoni kwa kuchelewa bado alishindwa kutimiza wajibu wake wa kitaaluma ikiwemo kutoa rufaa kwa mgonjwa kwenda kuhudumiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni (ambayo ipo takribani kilometa kutoka Kituo cha Afya Kabuku) baada ya mtaalamu wa usingizi kutopatikana kwenye simu na hivyo mgonjwa kutofanyiwa upasuaji kwa wakati.

"Kamati imebaini kuwa Daktari huyu alishindwa kutoa Taarifa ya dharura hii kwa Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya au Mganga Mkuu wa Halmashauri ili wawezi kuchukua hatua za haraka kwa ajili ya kuokoa maisha ya mama huyu." Alisema Waziri Ummy

Aidha Kamati ilibaini ukiukwaji wa Maadili kwa Muuguzi xxx mwenye utaalamu wa kutoa huduma ya dawa ya usingizi ambapo imepelekea kutakiwa kutoa maelezo ndani ya siku 14.



# Mpango mpya wa kutokomeza VVU, magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini wazinduliwa

**Na. Shaban Juma**
**Dar Es Salaam**

Mpango Mpya wa Kudhibiti UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini (NASHCoP) umezinduliwa leo rasmi ambapo umekabidhiwa dhamana ya kutokomeza maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi Nchini.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alizindua mpango huo Jijini Dar es salaam ambapo alisema licha ya mafanikio ya iliyokuwa Mpango taifa wa kuzibiti Ukimwi lakini bado kuna changamoto ya maambikizi mapya.

“Bado tuna kazi ya kufanya hususani kupunguza na kutokomeza maambukizi mapya ya VVU kwa vijana wenye umri wa miaka 15-24 na pia kutokomeza maambukizi mapya ya kutoka kwa mama kwenda kwa Mtoto, haiwezekani katika karne hii kwa kweli pamoja na wataalam tulionao, Rasilimali, dawa tushindwe kuitokomeza hii hali". Alisema Waziri Ummy.

Pia alisisitiza NASHCoP kwa kushirikiana na jamii kuendelea kuhimizana na kuhimiza makundi yaliyo katika hatari zaidi kama vile wasichana na wavulana walio katika rika balehe kuzingatia huduma jumuishi.

“Wanawake na vijana, akinamama wajawazito na wanaonyonyesha pamoja na watoto wao kwenda kupata huduma Jumuishi. Wataalamu wetu na jamii inayotuzunguka kufuatilia kutoa huduma hizo kwa weledi kulingana na miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya". alisema Waziri Ummy.

Aidha, Waziri Ummy aligusia suala la Magonjwa yasiyo ambukizwa na kusisitiza jamii kuchuka tahadhari juu ya magonjwa hayo yatokanayo mtindo wa maisha na chakula.

“Huu ndio ukweli ukiwa na UKIMWI na ukazingatia dawa unaishi vizuri kuliko ukiwa na sukari au presha ya damu, tuogope magonjwa yasiyo ya kuambukiza na tuwe na tahadhari nayo”. Alisema Waziri Ummy.



# Serikali kuendelea kuimarisha upatikanaji wa rasilimali watu katika sekta ya Afya

**Na. Cletus Sanga, Dodoma**

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo pamoja asasi za kiraia imepanga kuendelea kumiarisha rasilimali watu katika sekta ya afya kwa kuajiri watumishi na kutumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii katika kufikisha huduma za afya kwa wananchi.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu wakati akifungua Mkutano wa 23 wa mwaka wa kitaalam wa mapitio ya mafanikio na changamoto katika sekta ya afya unaoendelea jijini Dodoma.

Dkt. Jingu alisema rasilimali watu ndiyo watendaji wakuu wa sekta ya afya hivyo mkutano huo umelenga kujadili upatikanaji wao sehemu ambapo kuna mapungufu lakini pia kuangalia namna ya kuwawezesha kufanya kazi kwa uadilifu wanapokua kwenye maeneo yao ya kazi.

“Uwepo wa rasilimali watu wa kutosha unaenda sambamba na utayari wa kukabiliana na changamoto pale zinapojitokeza hivyo tunataka tujenge utayari wetu wa kutosha ili majanga yanapoingia nchini yakute tukiwa tumejikamilisha”. Alisema Dkt. Jingu.

Aidha, Dkt. Jingu aliongeza kuwa Serikali chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imewekeza vya kutosha kwenye sekta ya afya ambapo miundombinu ya afya imejengwa maeneo mengi nchini, hivyo Serikali ina wajibu wa kuhakikisha huduma za afya zinapatikana katika maeneo hayo kwa kupeleka vifaa tiba pamoja na watumishi wenye ujuzi na weledi wa kutosha.

Katibu mkuu huyo aliongeza kuwa katika Mkutano huo utajadili mafanikio na changamoto zilizopatikana katika kipindi cha mwaka 2021-2022 ili kuendeleza pale palipofanikiwa na kuweka mikakati mathubuti kwenye changamoto zilizojitokeza.

Kwa upande mwingine Dkt. Jingu alisema katika nchi kujiweka tayari na changamoto za afya zinazoweza kujitokeza, Serikali imeamua kuwatumia watumishi wa afya ngazi ya jamii (CHW) kuona nini kinachoendelea katika jamii yao kuweza kuwa chachu katika kuhamasisha jamii kushughulikia changamoto zilizopo katika maeneo yao.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa OR-TAMISEMI anayeshughulikia Afya Dkt. Wilson Mahela alisema Mkutano huo ni muhimu wa kujifanyia tathmini ya utoaji huduma katika Vituo vya huduma kuanzia ngazi ya msingi.





# Wahandisi wa vifaa tiba na wataalamu wa afya tunzeni vifaa kwa maendeleo ya sekta ya afya

**Na Shaban Juma**
**Dodoma**

Wahandisi wa Vifaaa Tiba na wataalam wa afya Nchini wametakiwa kulinda na kutunza vifaa vya kisasa ambavyo Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuwekeza na kupunguza uhaba wa Vifaa vya huduma za Afya hapa nchini.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Mafunzo Wizara ya Afya, Dkt. Saitore Laizer wakati akimuawakilisha Waziri wa Afya, katika ufunguzi wa Kongamano la pili la Wahandisi wa Vifaa Tiba, Jijini Dodoma.

Dkt Laizer alisema utunzaji wa vifaa hivyo utasidia serikali kupunguza adha na gharama za Matengezo ya vifaa hivyo na fedha ambazo zingesaidia kuleta maendeleo kwenye kada nyingine.

"Wahandisi wa Vifaa Tiba mnatakiwa kuvilinda na kuvitunza kwasababu Serikali imewekeza na kuboresha miundombinu ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza kwa kununua vifaa tiba, kuvisimika na kutoa elimu kwa wataalam wa afya namna ya matumizi bora ya vifaa" alisisitiza Dkt. Laizer.

Dkt. Laizer aliongeza kuwa Serikali licha ya kuwekeza vifaa vya kisasa bado imeendelea kupunguza uhaba wa wataalamu, watoa huduma za Afya na wataalam wa kufanya matengenezo na kurabati mitambo ya Tiba.

"Katika kipindi cha 2021 na 2023 jumla ya wataalam zaidi ya 280 wa kada ya Uhandisi wa vifaa tiba wameajiriwa. kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza afua zenye lengo la kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Sekta ya Afya ikiwa ni pamoja na kujenga na kukarabati karakana za ufundi wa vifaa tiba na ununuzi wa vitendea kazi katika ngazi mbalimbali" alieleza Dkt. Laizer

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Prof. Mohamed Janabi alipongeza baadhi ya vyuo kwa kuona haja ya kuanzisha kozi ambazo zinamsaada katika Sekta ya Afya Nchini huku akisisitiza umuhimu wa kuwekeza katika kujiendeleza kielimu wataalam na Wahandisi wa Vifaa Tiba Nchini.

# Waziri Ummy akabidhi vifaa vyenye thamani ya tsh: mil. 156 kwa waraibu Tanga



**Na Hassan Kimweri**
**Tanga**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu ambae pia ni Mbunge wa Jimbo la Tanga mjini amekabidhi vifaa vyenye thamani ya Tsh: Mil. 156 ambavyo vinalenga kuharakisha uponaji wa waraibu ambao wamepata nafuu baada ya kuacha kutumia madawa ya kulevya ili kuwawezesha kupata ujuzi wa kufanya kazi za ujasiliamali na kujitegemea.

Waziri Ummy alikabidhi vifaa hivyo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa (Bombo) kwa Mganga Mkuu wa Mkoa ambaye naye atakabidhi kwa walengwa ambapo alisema kuwa vijana wakitumia fursa hii vizuri wataweza kushiriki katika kazi za uzalishaji mali na kuaminika kwenye jamii.

Miongoni mwa vifaa vilivyokabidhiwa na Waziri Ummy ni pamoja na kits za aluminium zenye thamani ya shilingi milioni 38, vyerehani 10 vyenye thamani ya shilingi milioni 48, mashine mbili za tofali zenye thamani ya shilingi milioni 70.

“Vifaa hivi vinalenga kuharakisha uponaji wa waraibu ambao wamepata nafuu ili kuwawezesha kupata ujuzi wa kufanya kazi za ujasiliamali, kujitegemea na kuinua kipato cha vijana na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla.” Alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alisema Katika awamu ijayo vifaa vya kuoshea magari (car wash) vyenye thamani ya shilingi milioni 90 vitakabidhiwa katika vituo vya Bombo, Mount Meru na Itega, na vifaa vya saloon za kike na kiume vyenye thamani ya shilingi milioni 61.9 vitakabidhiwa mnamo Desemba, 2023.

“Vifaa ninavyokabidhi leo vinathamani ya Milioni Mia Moja na Hamsini na Sita (Tsh. Mil 156) na vifaa hivyo vitakavyo kabidhiwa awamu ijayo vitakua na thamani ya takribani milioni mia nne na ishirini na tano (Tsh. Mil 425).” Alisema Waziri Ummy

Mwisho, Waziri Ummy alimshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwajali Watanzania katika kuboresha na kuimarisha huduma za Afya pamoja na Wadau katika Sekta ya Afya kwa kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma za Afya hapa Nchini. Aidha amewataka vijana kujiepusha kutumia madawa ya kulevya na wale ambao wanatumia basi waende kujiandikisha kwenye vituo ili kupata huduma za matibabu ambayo yanatolewa bure na Serikali



# Waganga wakuu wa mikoa na wilaya jumuisheni afua za kifua kikuu na ukoma wakati wa afua nyingine

**Na. Majid Abdulkarim,**
**Dar Es Salaam.**

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amewaagiza Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha wanajumuisha huduma za Kifua Kikuu na Ukoma kwenye shughuli zao wanazotekeleza ili kuongeza nguvu za kudhibiti Magonjwa hayo ifikapo Mwaka 2030.

Dkt. Mollel alisema hayo kwenye Mkutano mkuu wa Mwaka wa wataalamu wa Kifua kikuu na Ukoma uliofanyika Mkoani Dar es Salaam huku akisisitiza hatari ya kuambukizwa kwa Zaidi ya watu laki nne kwa mwaka.

"Naagiza waganga wakuu wa Mikoa na Wilaya katika shughuli zenu mjumuishe Ukoma na Kifua Kikuu, nikienda kila mkoa nitaangalia ni namna gani waratibu wa mikoa na wilaya wanavyoshirikishwa kwenye shughuli zinazofanyika kwa rasilinali hizo hizo zilizopo". Alisema Dkt. Mollel

Pia, Dkt. Mollel alisema kwa takwimu za Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Kifua kikuu na Ukoma, mgonjwa mmoja wa kifua kikuu ambaye hakupata matibabu anauwezo wa kuambukiza watu 15 hadi 20 kwa mwaka mmoja.

"Kutokana na wagonjwa 27,033 wenye maambukizi ya Kifua Kikuu kutopatikana kuanza tiba ya ugonjwa huo, kuna hatari ya watu 407,225 kuambukizwa kifua kikuu ndani ya mwaka mmoja" Alisema Dkt. Mollel

Akieleza mikakati ya kutokomeza Kifua kikuu nchini, Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dk John Jingu kupitia taarifa yake iliyosomwa na mwakilishi wake Catherine Joachim alisema Tanzania imewekewa lengo na Umoja wa Mataifa kutokomeza maambukizi ya kifua kikuu kufikia 2030

"Lengo ni asilimia 90 ya walioanzoshiwa dawa wawe wamepona hapa asilimia 95 tuliowaanzishia dawa wamepona, na tumepunguza vifo kwa asilimia 69 ya lengo la asilimia 90 tuliyojiwekea,"alisema.

Lengo la kujumuisha magonjwa ya Kifua kikuu na Ukoma kwenye shughuli zinazofanywa na waganga wakuu mikoa na wilaya ni kuendelea kuibua wagonjwa wa kifua kikuu ambao bado hawajaanza tiba

# Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri simamieni huduma za matibabu ya Meno kabla ya kufikia kung'oa

**Na Hassan Kimweri,**
**Newyork USA.**

Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri wametakiwa kuhakikisha wanasimamia matibabu bora ya Kinywa na Meno na kupunguza kung'oa meno bali waongeze watu wanaotibiwa meno.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema hayo wakati akifungua Kongamano la 38 la kisayansi la Kitaifa na mkutano mkuu wa mwaka wa chama cha wataalam wa Afya ya Kinywa na Meno linalofanyika Jijini Tanga.

"Mbali na Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri lakini pia Hospitali zote za umma zinazotoa matibabu ya Kinywa na Meno zihakikishe zinaboresha miundombinu ya kliniki za Kinywa na Meno pamoja na kununua vifaa vya kisasa." Alisema Waziri Ummy.

Aidha, Waziri Ummy alisema kuwa Takwimu za kuziba meno zimeongezeka kutoka asilimia 2 mwaka 2020 mpaka asilimia 36.1 mwaka 2023 ambapo hali hii imetokana na uwekezaji wa Serikali ya awamu Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema, Takwimu za Mwaka 2022/2023 zinaonesha kuwa watu 541,159 waliooza meno yao ambapo watu 174,749 sawa na 32.3% walizibwa meno yao na watu 323,419 sawa na 59.8% waling'olewa meno yao.

"Kuna Mikoa na Wilaya ambazo zimevuka 60%, nataka nione takwimu za kuziba meno zikiendelea kuongezeka na takwimu za kung'oa meno zikipungua, hali hii iende sambamba na utoaji wa elimu ya kinywa na meno kwa ajili ya kuzuia magonjwa yatokanayo na kukosa elimu sahihi ya kujikinga na magonjwa hayo." Alisema Waziri Ummy.

Hata hivyo, Waziri Ummy alisema Sambamba na uwekezaji huo, Serikali imeongeza ufadhili wa wataalam wa Sekta ya Afya hasa nafasi za kibingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi kwa kutenga shilingi bilioni 8 ambapo kati ya hizo Tsh. Bil 3 zimetengwa kwa ajili ya kusomesha wataalam kwa seti ili kuleta ufanisi wakati wa utoaji huduma za kibingwa bobezi za Afya.



# "Tuunge mkono kwa vitendo jitihada za Dkt. Samia katika sekta ya Afya ", Dkt. Mollel



**Na Hassan Kimweri**
**Dar Es Salaam.**

Uwekezaji wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mhe Dkt Samia Suluhu Hassan katika Sekta ya Afya utaongeza tija iwapo wahudumu wa Sekta ya Afya nchini watatoa huduma bora zenye tija kwa wananchi.

Hayo yalibainishwa na Naibu Waziri wa Afya Dkt Godwin Mollel wakati akizungumza na watumishi wa hosptali ya Rufaa ya mkoa ya Mwananyamala wakati wa ziara yake ya kikazi

Dkt. Mollel aliwasisitiza watumishi wa kada ya afya nchini kuhakikisha wanaboresha huduma kwa kufuata misingi ya huduma kwa wateja ili wagonjwa wapatiwe huduma bora kuanzia waingiapo hospitalini

Dkt. Mollel alisema, baadhi ya wananchi hawafiki hosptali za serikali kutokana na kukosekana kwa huduma rafiki kwa wateja na kutaka pia walinzi wajengewe uwezo wa kujua namna bora ya kupokea wagonjwa badala ya kufokea ndugu za wagonjwa au wagonjwa wenyewe

"tuna kazi moja ya kuhakikisha tunaboresha huduma kwa mteja, lugha zetu na kila kitu kikae vizuri", alieleza Dkt. Mollel

Alitoa wito kuwa wajipange vizuri kwenye eneo la huduma kwa mteja ili kuleta tija ya uwekezaji uliofanywa na rais dkt samia suluhu hassan katika Sekta ya Afya nchini .

Aidha Dkt. Mollel alisema kwa kipindi hiki Rais DkT. Samia Suluhu Hassan adaiwi chochote katika Sekta ya aAfya, bali watoa huduma ndio wanadaiwa kutoa huduma bora kwa wananchi





# Viongozi wa sekta ya afya simamieni ubora wa huduma za afya nchini

**Na. Majid Abdulkarim,**
**Dar Es Salaam**

Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Molel, amewataka Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha wanasimamia ubora wa huduma katika Hospitali na Vituo vya kutolea Huduma za afya na kuhakikisha wanawajengea uwezo watumishi ili kuepuka changamoto na uzembe unaofanywa na baadhi ya wataalamu wa afya nchini.

Dkt. Mollel alitoa agizo hilo Jijini Dar Es Salaam wakati akizungumza na watumishii wa afya katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke.

Dk. Mollel alisema yanapotokea matatizo katika vituo vya afya alafu Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya hawana taarifa au hawajachukua hatua hadi viongozi wa taifa wanafika watu hao wanatakiwa wajitafakari.

Alisema yanapotokea matatizo katika sekta ya afya pamoja na daktari aliyefanya uzembe watu wengine watakao kuwa watuhumiwa ni waganga wakuu wa wilaya na mikoa kwa kutoona na kutatua changamoto kabla hazijatokea.

“Tukija kwenye mkoa wako tukakuta uzembe umetokea mama mjamzito amefariki na Mganga Mkuu wa Wilaya na Mkoa ni mtuhumiwa mpaka vyombo vitakapo chunguza, tukikuta mama, mtoto au mtu yoyote amepata shida alafu mganga mkuu wa mkoa, wilaya na wewe unashangaa inabidi ujitafakari". Alisema

Aidha, aliwataka watoa huduma na wataalamu wa afya kutunza vizuri vifaa tiba vinavyotolewa na Serikali kwani Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amefanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya afya nchini.

Hata hivyo alisema kuwa Rais Dk. Samia ameshafanya kazi yake ya kuwekeza katika sekta ya afya kwa kununua vitendea kazi vingi, ikiwemo kuwekwa mashine za CT Scan ili mtanzania apate huduma bora.



# Matumizi ya vyoo bora yameongezeka nchini Tanzania

**Na. Emmanuel Malegi**
**Dar es salaam**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema Tanzania imekua na ongezeko kubwa la watu wanao tumia vyoo bora kutoka asilimia 21 mwaka 2016 hadi asilimia 74.8 mwaka 2022 ambapo ni hatua chanya ya kufikia lengo la 6.2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya 2030 "Sustainable Development Goals".

Waziri Ummy alisema hayo katika tamko lake likionesha hali ya matumizi ya vyoo nchini ambapo mikoa inayoongoza kwa matumizi ya vyoo bora ni Dar es Salaam (98.5%), Ruvuma (92.1%) na Njombe(87.6%).

Aidha, Waziri ummy alisema Licha ya kuwa tumepiga hatua kwenye kiashiria hicho bado kuna baadhi ya watu hawatumii vyoo ambapo takwimu zinaonesha kuwa asilimia 9.8 ya watu nchini hawana vyoo kabisa ambapo hali ni mbaya zaidi maeneo ya vijijini.

"Kwa mujibu wa taarifa hii asilimia 13.4 ya wakazi wa vijijini hawana vyoo kabisa. Tafsiri ya kiashiria hiki ni kwamba watu hawa ndiyo wanaojisaidia ovyo (Open defecation) vichakani na maeneo mengine ambayo sio rasmi hali hii inachangia kuwepo kwa magonjwa ya milipuko ikiwemo kipindupindu ambapo kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba 2023 jumla ya watu 749 waliougua na 16 kupoteza Maisha". Alisema Waziri Ummy.

Hata hivyo Waziri Ummy alibainisha mikoa inayoongoza kwa kutokuwa na vyoo ni Katavi (24.3%), Simiyu (24.3%) na Manyara (22.3%) huku akiagiza Sekretatarieti za Mikoa na Halmashauri kuhakikisha kaya zote nchini zinakuwa na vyoo bora.

Waziri Ummy aliielekeza Mikoa na Halmashauri kutekeleza kufanya ukaguzi kwenye kaya, sehemu za Jumuiya, maeneo ya biashara na Taasisi zote kwa kuhakikisha zinajenga na kutumia vyoo bora pia Kusimamia vyema Sheria ya Afya ya Jamii na Sheria Ndogo zinahusiana na ujenzi na matumizi ya choo bora kwenye ngazi ya Kaya, Taasisi na maeneo ya Jumuiya.

Vile vile alielekeza kuhakikisha zinasimamia vyema matumizi ya vyoo kwa wasafiri wawapo safarini kwa kuhakikisha mabasi yanasimama kwenye maeneo rasmi ikiwemo stendi za mabasi na vituo maalum pamoja na kupiga marufuku tabia ya wasafiri kujisaidia hovyo maarufu kama kuchimba dawa kwani ni aibu kwa Taifa na pia udhalilishaji wa utu.

# Viongozi wa hospitali na timu za afya simamieni ubora wa huduma za afya kwa wananchi

**Na. Emmanuel Malegi**
**Dar es salaam**

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amewataka viongozi wa Hospitali zote na Timu za Afya nchini kuhakikisha wanasimamia ubora wa Huduma za afya kwa wananchi kwani Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imewekeza fedha nyingi katika sekta ya afya nchini.

Dkt. Mollel alielekeza hayo Jijini Dar Es Salaam katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Magonjwa yasiyoyakuambukiza yaliyofanyika katika viwanja vya Hospitali ya Mnazi Mmoja

Aidha Dkt. Mollel alisema kuwa ili kuleta tija kwa uwekezaji uliofanywa na Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan waganga Wakuu wa mikoa na halmashauri nchini wanatakiwa kuhakikisha wanasimamia vyema ubora wa Huduma za afya katika maeneo yao

“Kwenye Kituo cha kutolea Huduma za afya kilichopo katika halmashauri au mkoa husika hakitoi Huduma bora kwa wananchi mtuhumiwa namba moja utakuwa ni mganga mkuu wa mkoa huo, alafu ndiyo tunaenda kuangalia yule alokosea”. Alisema Dkt. Mollel

Aidha Dkt. Mollel alitoa wito kwa watanzania wote kuhakikisha wanawekeza nguvu kubwa katika kutunza mazingira ili kuepuka milipuko ya magonjwa mbalimbali kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha hapa nchini.

“Mvua zinazonyesha kama mazingira sio rafiki maji yatatuama na kusababisha mbu kuzaliana na kuleta malaria lakini pia kama usafi wa mazingira sio mzuri unaweza sababisha kipindupindu”. Alisema Dkt. Mollel

Hata hivyo Dkt. Mollel alitoa rai ya wananchi kujenga utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara, kufuata utaratibu na ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya kwa kuzingatia ulaji bora ili kuepukana na magonjwa yasiyo yakuambukiza



# Onyo kwa wafamasia wanaouza Dawa bila cheti cha Daktari

**Na Shaban Juma**
**Arusha**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu ametoa onyo kali kwa wafamasi na wamiliki wa maduka ya dawa waotoa dawa bila kuangalia cheti cha daktari kwa kuwa kufanya hivyo ni kuendeleza tatizo la usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na kuhatarisha afya za watu.

Waziri Ummy alisema hayo wakati akifunga Kongamano la Tatu la Usugu wa Vimelea dhidi ya Dawa na kufungua rasmi wiki ya uhamasishaji na uelimishaji jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa iliyoanza Novemba 18 hadi 24, 2023.

"Nataka wafamasia wote nchini kuacha mara moja tabia ya kutoa dawa ikiwemo za Antibiotiki bila cheti cha daktari na nikimkamata mtu siku moja nitampiga faini kubwa kama sio kumfungia duka kabisa." Alisema Waziri Ummy.

Alisema, atatuma timu kufanya kaguzi za kushtukiza kwenye maduka ya dawa, ambapo amesisitiza mfamasia atakaebainika kutoa dawa za Antibiotikibila cheti cha daktari atafikishwa mahakamani na atalipa faini kubwa.

Aidha, Waziri Ummy aliwataka wataalamu wa Afya kuzingatia Mwongozo wa Taifa wa Matibabu wanapo wahudumia wagonjwa ili kufanikisha kampeni ya 'Afya Moja' yenye lengo la mapambano ya Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi ya Dawa.

"Naendelea kusisitiza kwa wataalam wetu wa Afya, hakikisheni mnazingatia Mwongozo wa Taifa wa Matibabu, nawaomba sana hasa katika kuwaandikia wagonjwa dawa, maana tumepata kesi tunaona mtu ana UTI anaandikiwa Antibiotic mpaka saba." Alisema Waziri Ummy

Alisema, iwapo watoa huduma za Afya watafuata Mwongozo wa Taifa wa Matibabu itawezesha Serikali kwenda kwa kasi katika mapambano ya Usugu wa vimelea dhidi ya dawa.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu aliwaasa wataalam wa kilimo, uvuvi, mifugo na afya kuzingatia dhana ya mwaka huu ya Kongamano hilo kwa kuendelea kuboresha njia za mapambano ya tatizo la usugu wa vimelea dhidi ya dawa na kutoa elimu ya uwelewa kwa jamii ili kufikia lengo la mpango huo.






# Tuongeze nguvu zaidi kupambana na Ugonjwa wa Kifua Kikuu ili tuutokomeze ifikapo 2030

**Na. Majid Abdulkarim,**
**Dar Es Salaam.**

Naibu Waziri wa Afya Dkt Godwin Mollel amewataka Waganga wafawidhi wa Hospitali zote nchini kuwajibika na kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili kuleta tija ya uwekezaji uliofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan katika sekta ya afya.

Dkt. Molel alitoa kauli hiyo alipofanya ziara katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kuangalia hali ya utoaji huduma za afya na kufanya mazungumzo na Wakuu wa Taasisi za Afya ikiwemo Hospitali ya taifa ya Muhimbili (MNH), Taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Mifupa MOI, Bohari ya Dawa (MSD), Shirika la Bima la taifa NHIF, Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba (TMDA), Mganga Mkuu wa mkoa pamoja na Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za mkoa wa Dar es saalam .

Dkt. Mollel alisema Serikali haitamvumilia kiongozi yoyote anayekwamisha juhudi za uboreshaji wa huduma katika sekta ya afya nchini kwani Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mapinduzi makubwa katika sekta ya afya hivyo ni jukumu la usimamizi imara ili kuleta ubora wa Huduma kwa wananchi

Aidha, Naibu Waziri wa Afya alieleza mafanikio katika uboreshaji wa huduma sio uwekezaji wa vifaa tiba na rasilimali watu pekee bali ni pamoja na kuwepo kwa uongozi bora na kila mmoja kutimiza wajibu wake.

"Mhe. Rais wa Awamu ya Sita Dkt.Samia Suluhu Hassan ameshamaliza kazi yake kwa kuwekeza Trilioni 6.7 katika miundombinu, taaluma, teknolojia tiba na rasilimali watu sasa ni wakati wa kila kiongozi kutekeleza majukumu yake

kwakua sera ya Wizara ya Afya kwasasa ni kuhakikisha Hospitali za Serikali zinatoa huduma bora zinazokidhi viwango". Alisema Dkt. Mollel

Dkt. Mollel alisema ziara yake ni kutokana na agizo la Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu kutembelea hospitali zote nchini juu ya kuangalia ubora wa huduma za afya kwa wananchi.

"Mhe. Waziri wa Afya Ummy Mwalimu ameniagiza kutembelea hospitali zote nchini kuangalia suala la ubora katika utoaji huduma na kufanya marekebisho katika maeneo ambayo hayafanyi vizuri, kiongozi kama hutekelezi majukumu yako inavyotakiwa unapaswa kujitafakari, hata hivyo napenda kuzipongeza Taasisi za MNH, MOI na JKCI kwa kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya afya". Alisisitiza Dkt. Mollel

Wakati huohuo Dkt. Mollel alisema Wizara ya Afya imedhamiria kuhakikisha kuwa mifumo ya TEHAMA katika hospitali kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa inasomana ili kumpunguzia muda mgonjwa wa kusubiri kupata matibabu kwa kurudia kufanya kipimo isipokua pale inapolazimu kurudia kufanya kipimo husika.

# Kwa matumizi sahihi ya lishe tumieni mwongozo wa taifa wa chakula na ulaji

**Na. Cletus Sanga**
**Dar Es Salaam**

Maafisa lishe, Wataalam wa Afya, Wataalam wanaotoa Elimu ya Lishe pamoja na Watafiti watakiwa kutumia Mwongozo wa Taifa wa Chakula na Ulaji kwa kutoa elimu ya masuala ya lishe kulingana na mwongozo unavyowataka.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema hayo wakati akizindua Mwongozo huo wa Taifa wa Chakula na Ulaji, uliandaliwa ili kuhamasisha matumizi sahihi ya Chakula mchanganyiko katika kutokomeza changamoto zote za Utapiamlo uliofanyika katika Soko la Kisutu Jijjni Dar es Salaam.

"Mwongozo huu unaweza kutumiwa na kila Mtanzania na umehakisi mazingira yaliyopo nchini, na unaenda kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 12 Barani Afrika kuwa na Mwongozo wake wa Chakula na Ulaji." Alisema Waziri Ummy.

Alisema, Watanzania wanahitaji sana Mwongozo huu kwa sababu bado kuna tatizo la lishe duni nchini na tatizo hilo limekuwa kisababishi kikubwa cha utapiamlo wa aina zote katika jamii na kuchangia kushindwa kufikia kwa malengo ya kiafya na kimaendeleo kwa mtu mmoja mmoja, kaya na taifa kwa ujumla.

"Nimeupitia Mwongozo huu nataka niwahakikishie Watanzania Mwongozo huu unaweza kutumiwa na kila Mtanzania, awe mjini, awe kijijini, awe tajiri, awe maskini, ni mwongozo ambao unahakisi mazingira ya Kitanzania." Alisema Waziri Ummy

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania Dkt. Germana Leyna alisema kiu kubwa ya Watanzania ilikuwa ni kufahamu ale chakula gani na chenye mchanganyiko upi na kwa kiasi gani, hivyo ujio wa Mwongozo wa Chakula na Ulaji unaenda kukidhi mahitaji hayo.

"Matumizi sahihi ya Mwongozo huu yanaenda kuleta tumaini la kuondokana na matatizo ya udumavu na kwenda kupunguza changamoto zinazoleta matatizo ya upungufu wa Madini na Vitamini kwa Watanzania." Alisema Dkt. Germana

Mwongozo wa taifa wa Chakula na Ulaji uliandaliwa na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ukiwa na malengo mahususi ya kuongeza matumizi sahihi ya chakula mchanganyika katika kaya, kuhamasisha kupunguza matumizi ya Chumvi, Sukari na Mafuta, Kuhamasisha usafi wa Mazingira yanayotumika kuandaa Chakula na kuboresha Afya na lishe za jamii.






# 70% ya magonjwa ya Binadamu yanatokana na wanyama

**Na. Englibert Kayombo**
**Arusha**

Wataalam wa Afya ya binadamu, Afya ya mifugo na jamii wametakiwa kushirikiana ili kupambana na asilimia 70 ya magonjwa ya binaadamu yatokanayo na wanyama.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega alisema wakati akifungua Kongamano la Tatu la Kisayansi la Mapambano ya Usugu wa Vimelea dhidi ya Dawa (UVIMADA) Jijini Arusha

Waziri Ulega alisema matumizi yaliyokithiri ya dawa za Antibiotiki katika kukuza mifugo kwa kuchanganya na chakula cha mifugo kwa matumizi ya kila siku kwa wanyama wanapokuwa hawaumwi hupelekea magonjwa kwa mlaji wa mfugo huo.

“Asilimia 70 ya magonjwa ya binadam yatokana na wanyama ambao nao huyatengeza kwa kupewa dawa za Antibiotiki bila utaratibu, tunapaswa kuchanja mifugo yetu kwa wakati ili iwe na kinga dhidi ya magonjwa na kuacha kuchinja mifugo inayoendelea na matibabu.” Alisema Waziri Ulega

Alisema ni wajibu wa kila mmoja kuhakikisha anapambana na asilimia 70 ya magonjwa ya binadam yatokanayo na matumizi ya Antibiotik yaliyokithiri.

“Tatizo hili ambalo ni tishio kwa kizazi chetu kijacho sababu matokeo ya tafiti mbalimbali za ukusanyaji wa taarifa za dawa nchini zinaonyesha kuwa takribani 60% ya dawa zote zinazotumika hapa nchini hutumiwa na sekta ya wanyama (mifugo na Uvuvi) ambapo mlaji wa mwisho ni Binadamu kwahiyo kaeni tengenezi mikakati ya pamoja kwa kushirikina na jamii, mje na mkakati utakaosaidia kulimaliza tatizo hili.” Alisema Waziri Ulega

Aidha, Waziri Ulega alitoa wito kwa wauzaji wa dawa na watengenezaji wa chakula katika kuchochea mapambano ya dawa dhidi ya vimelea sugu vya magonjwa.

Kwa upande wake Prof. Robinson Mdegela kutoka Chuo kikuu cha Sokoine cha kilimo (SUA) wakati akitoa mada alisema tatizo la usugu wa vimelea dhidi ya dawa ni changamoto mtambuka na ni vema tuzidishe juhudi katika kupambanna nalo.
“Dunia kote tumekubaliana kuja na dhana ya Afya Moja ili kuunganisha nguvu kupambana na hili, namna ya kupambana ni kufanya tathmini kwa tulipofikia ambapo changamoto utaona ni elimu kwahiyo tuelimishe watu ili wajue na kisha kuliepuka.” Alisema Prof. Mdegela



# Wataalam, wasimamizi na watoa hudumaza afya zingatieni viapo vya taaluma na weledi.

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**Morogoro**

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu amewataka wasimamizi na watoa huduma za afya nchini kote kuhakikisha wanatoa huduma kwa kuzingatia viapo vya taaluma zao, maadili ya kazi na weledi katika kuwahudumia wagonjwa ili kuokoa maisha ya watanzania na taifa kuwa na afya bora kwa ujumla

Dkt. Jingu alitoa wito huo wakati akizungumza na watumishi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro ambapo alisema serikali haitasita kuwachukulia hatua wale wote wawatakao kiuka taratibu na kanuni za kazi kwani wanakwamisha jitihada za serikali ya awamu ya sita katika kuendelea kuboresha huduma za afya za watanzania.

“Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan lengo letu kubwa kuokoa, kulinda maisha, kuleta unafuu na ahueni kwa wanaoteseka na magonjwa mbalimbali, kama daktari au muuguzi unajua miiko yako ya kazi ni ipi ili kufanya kazi kwa kuzingatia viapo vya taaluma zenu ili kuleta tija kwa wananchi kupata huduma bora", alisisitiza Dkt. Jingu.

Pia Dkt. Jingu aliwataka wahudumu na wasimamizi hao kutambua umuhimu wa jukumu ambalo wamekabidhiwa ili kuweza kufikia malengo ya serikali katika kuwahudumia wananchi

Aidha Dkt Jingu alisema Serikali haitasita kumchukulia hatua msimamizi au mtoa huduma za Afya yoyote ambaye ataonekana kukiuka viapo vya taaluma na maadili ya kazi

“Serikali haya mambo hatuwezi kuyavumilia lazima tuyashughulikie kwa nguvu zote za kisheria, kwa kuchukua hatua kali kwa wote wanaofanya uzembe kwa sababu kosa moja dogo tu linaweza kusababisha mtu kupoteza maisha ama mtu kupata kilema cha kudumu, Kwahiyo ni lazima tufanye kazi kwa kuzingatia maadili na tusikubali uzembe upite kati yetu” aliongeza Dkt. Jingu

Naye Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu aliwashukuru na kuwapongezi watoa huduma za afya katika Hospitali kwa kutambua kazi kubwa wanayoifanya ya kuwahudumia watanzania ili kuwa na taifa lenye afya bora.



# Rais Kikwete aipongeza serikali kwa juhudi za kupunguza vifo vya akinamama wajawazito

**Na. Emmanuel Malegi**
**Dar Es Salaam**

Rais Mstaafu wa awamu ya nne Dkt. Jakaya Kikwete ameipongeza Serikali kwa kufanikiwa kupunguza vifo vya akinamama wajawazito kutoka vifo 556 556 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 104 mwaka 2022.

Dkt. Kikwete alisema hayo wakati akifungua kongamano la pili la kisayansi la afya ya uzazi mama na mtoto ambalo linafanyika jijini Dar Es Salaam linalojumuisha wataalam mbalimbali wa sekta ya afya.

Dkt. alisema mwaka 2000 hadi 2015 katika malengo ya Milenia yalitaka nchi zinazoendelea kupunguza vifo vya akinamama wajawazito kufikia 191 kwa kila vizazi hai laki moja, lakini Tanzania mwaka 2015 tulifikia vifo 432 katika vizazi hai laki moja na vikaendelea kuongezeka hadi kufikia 556 mwaka 2016.

"Mwelekeo wa sasa wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi ni mzuri, vifo vimepungua kutoka 556 mwaka 2016 hadi kufikia 104. Hii ni hatua kubwa naipongeza

Serikali na Wizara ya Afya kwa jitihada ilizoweka, ni jambo la kufedhehesha kuona mama ambaye analeta uhai wa kiumbe duniani anapoteza maisha". Alisema Jakaya Kikwete.

Kwa upande wake Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alimshukuru Dkt. Kikwete katika awamu yake ya uongozi kwa kutambua na kuthamini huduma za afya ya uzazi ambapo mwaka 2014 alizindua mpango wa kuchochea huduma bora za afya ya uzazi ili kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na Watoto.

Aidha, Waziri Ummy alimshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake katika kuboresha huduma bora za afya kwa Watanzania katika ujenzi wa miundombinu ya afya katika maeneo mengi, upatikanaji wa vifaa na vifaa tiba, kuajiri watumishi wa afya pamoja na kujengea uwezo watumishi wa afya.

Hata hivyo, akitolea mfano wa kifo cha mama mjamzito kilichotokea hivi karibuni Mkoani Tanga, Waziri Ummy alitoa wito kwa watumishi wa afya watakaoshindwa kutimiza majukumu yao kazini kuwa hatasita kuchukua hatua za kuwafutia usajili madaktari na manesi watakaobainika kuhusika na kifo hicho huku akiongeza kuwa hatua zilizochukuliwa hivi sasa ni za kiutawala ambazo wanaotuhumiwa wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi.

# Dkt. Jingu akoshwa na huduma zinazotolewa hospitali ya mkoa morogoro

**Na, Abdulwaheed Madenge**
**Morogoro**

Huduma zinazotolewa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro zinaenda sambamba na malengo ya Sekta ya Afya kwa kutoa huduma zinazozingatia mipango ya uboreshaji wa huduma za Afya nchini.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu alisema hayo wakati akizungumza na watumishi na watoa huduma za Afya katika Hospitali hiyo.

Dkt. Jingu alitembelea wodi mbalimbali ikiwemo wodi ya uangalizi maalum ya watoto, wodi ya wanaume ya upasuaji wa mifupa, wodi ya watoto pamoja na wodi ya watoto njiti ambapo amezungumza na wagonjwa wakimueleza huduma nzuri wanazopata katika Hospitali hiyo.

“Kwakweli nimezunguka wodi mbalimbali katika Hospitali hii ikiwemo wodi ya watoto njiti na nimeona huduma nzuri na

Aidha, Dkt. Jingu pamoja na kutoa pongezi kwa watumishi hao aliwataka kuendelea kutoa huduma kwa kuzingatia taaluma zao, maadili ya kazi pamoja na weledi katika kuwahudumia wagonjwa.

“Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaimani na ninyi hivyo kuendelea Imani hiyo kwa Mhe. Rais mnatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia maadili, weledi na taaluma mliyokuwa nayo ili kuleta ahueni na nafuu kwa wanaoteswa na Magonjwa mbalimbali.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu aliwashukuru na kuwapongezi watoa huduma wote wa Hospitali kwa kutambua kazi kubwa wanayoifanya kwakuwa kazi hiyo ni yenye thawabu nyingi.

“Tunatambua kuwa kazi ya kumhudumia mgonjwa unaweza kupata sifa nzuri au lawama au laana hivyo ni vyema kuzingatia majukumu yetu wakati wa kazi kwa kufuata taratibu na miongozo ya taaluma zetu.” Alisema Prof. Nagu



# Hadubini 133 zakabidhiwa kwa ajili ya vyuo vya afya vya kati na vituo vya tafiti za magonjwa ya binadamu



**Na. Said Nyaoza,**
**Dar Es Salaam.**

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani, kupitia Shirika la Mandeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) na Mpango wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria (PMI), imekabidhi Hadubini 133 na vitendanishi vingine vya maabara vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi za kitanzania Bilioni 1.2 kwa ajili ya kutumika kufundishia katika vyuo vya Wizara ya Afya vinavyo toa kozi za maabara katika Mikoa sita ambayo ni Mbeya, Morogoro, Dar es Salaam, Tanga, Mara, na Singida.

Hafla ya makabidhiano ya vifaa hivyo iliyofanyika katika chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUCOHAS) Jijini Dar es Salaam na kushuhudiwa na Mkuu wa Program kutoka Wizara ya Afya Dkt. Catherine Joachim akimuwakilisha Mganga Mkuu wa Serikali.

Dkt. Catherine alisema Hadubini hizo zitasaidia kukuza uwezo wa wataalamu wa maabara kwa kuweza kutambua kwa usahihi vimelea vya malaria kwa kuthibitisha uwepo wa vimelea hivyo ili kuwezesha wagonjwa kuanza matibabu sahihi na kwa wakati.

"Hadubini hizi na vitendanishi vingine vya maabara vilivyotolewa leo vitawezesha Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kuimarisha uwezo wa kimaabara katika chunguzi na kusaidia utoaji matibabu ipasavyo, itakayopelekea kuokoa maisha ya watu na kuzuia madhara ya malaria". Alisema Dkt Catherine

Nae Meneja Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria Dkt. Samwel Lazaro aliishukuru Serikali ya marekani kwa kupata hadubini kwenda kwenye vyuo vya afya kwani ndio asilimia kubwa wana ajiriwa kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya

Kwa upande wake Mkurugenzi wa ofisi ya Afya kutoka USAID Tanzania Bi. Anne Murphy aliipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Afya kwa juhudi zake zilizopelekea kupungua kwa kasi kiwango cha malaria nchini Tanzania kutoka zaidi ya asilimia 14 ya watu mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 8 tu mwaka 2022.

# Wakurugenzi kununua viatilifu vya kuulia mazalia ya mbu

**Na.Cletus Sanga**
**Dodoma**

Wakurugenzi wa Halmashauri ya mkoa wa Tabora wametakiwa kununua viatilifu vya kuua mazalia ya mbu na viluilui kwa mapato yao ya ndani ili kupunguza idadi ya maambukizi ya ugonjwa wa Malaria.

Hayo yalisemwa na Balozi Dkt. Batilda Buriani wakati akiwapokea Wabunge wanaounda Mtandao wa Wabunge wanaopambana na Malaria na Magonjwa yasiyopewa Kipaumbele (TAPAMA) wakifanya ziara kuangalia hali ya huduma na maendeleo ya mapambano dhidi magonjwa hayo katika Mkoa wa Tabora.

Dkt. Batilda alibainisha hatua za kukabiliana na ugonjwa wa malaria ikiwa ni Pamoja na kuwataka wakurugenzi kununua viatilifu vya kuua mazalia ya mbu na viluilui Pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutumia chandarua na kua na utaratibu wa kwenda kutibiwa hospitali.

Aidha Dkt. Batilda alielezea kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa Malaria katika mkoa wa Tabora kilikua ni 11.7% kwa Watoto kati ya umri wa miezi 6 hadi 59 kwa mwaka 2017/2018 hivyo kuongezeka hadi 23.4% hivyo kufanya mkoa wa Tabora kuwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya Malaria katika Jamii.

"Jiografia ya mkoa wa Tabora kuwa na maeneno mengi yenye madimbwi ya maji yanayotuama katika maeneo mbalimbali ya makazi ya watu hasa kwenye kipindi cha mvua zimechangia kuwa na kiwango cha juu cha maambukizi ya Malaria". Alisema Dkt. Batilda.

Pia, Dkt. Batilda alisema kuwa Imani potofu iliyojengeka katika jamii juu ya matumizi ya vyandarua vyenye dawa imeongeza hali ya maambukizi ya Malaria hali iliyopelekea baadhi ya wananchi kutotumia vyandarua wanavyogawiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya hivyo kutoa wito kwa jamii kufika katika kituo cha huduma za afya kwa ajili ya matibabu badala ya waganga wa kienyeji.

Dkt. Batilda aliishukuru Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiongezea bajeti ya dawa Mkoa wa Tabora kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa mbali mbali.





# Waziri Ummy ataka ripoti ya kifo cha mjamzito na kichanga ndani ya siku 7

**Na. Englibert Kayombo,**
**Tanga.**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu ametoa maelekezo kwa Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania (TNMC) kuhakikisha ndani ya Siku 7 wamempelekea taarifa ya tukio la kifo cha mjamzito na kichanga chake kilichotokea tarehe 11 Novemba 2023 Mkoani Tanga.

Alisema, tayari hatua za awali zimeshachukuliwa ikiwemo ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe. Waziri Kindamba kutuma timu kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa inayojumuisha Madaktari bingwa wawili akiwemo Daktari Bingwa wa Wanawake na Uzazi na Daktari Bingwa wa Huduma za Usingizi ili kufanya uchunguzi wa tukio hili.

“Hatua nyingine iliyochukuliwa baada ya tukio hilo ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kuwasimamisha kazi watumishi watatu (3) walioshiriki kumpatia huduma mama huyo tangu alipopokelewa kituoni hadi umauti ulipomkuta ili kupisha uchunguzi wa tukio hili baya na lisilopaswa kuvumiliwa.” Alisema Waziri Ummy

Pia Waziri Ummy aliwahakikishia Watanzania kuwa baada ya kupokea taarifa ya Uchunguzi, kila mtumishi aliyehusika atachukuliwa hatua kali za kitaaluma, kiutumishi na kijinai ikiwemo kufikishwa Mahakamani kujibu tuhuma za kijinai pale itakapothibitika.

Mwisho, Waziri Ummy alitoa pole kwa familia iliyoguswa na msiba huu na ameahidi kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya itaendelea kusimamia ubora wa huduma za Afya ili kufikia matarajio ya wananchi wote.

# Hakikisheni takwimu sahihi zinapatikana kusaidia mipango ya maendeleo ya sekta ya afya

**Na. Abdulwaheed Madenge, Morogoro**

Waratibu wa Mfumo wa Takwimu wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya Nchini (HMIS) wametakiwa kuhakikisha ukusanyaji wa takwimu kwa kutumia mifumo ya kielektroniki unafikia vituo vyote vya kutolea huduma za Afya.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu alisema hayo wakati akifungua mkutano wa mwaka wa waratibu wa takwimu za Afya Mkoani Morogoro.

"Hakikisheni mnaimarisha ustadi wa kuchambua takwimu na kufikisha matokeo kwa wananchi kwa wakati ili takwimu sahihi zitumike katika Mipango mbalimbali ya Maendeleo na tunatakiwa kuwa na mifumo michache ya takwimu inayosomana ili kupunguza gharama kwa Serikali." Alisema Dkt. Jingu

Aidha, Dkt. Jingu alisema kuwa takwimu zote zinazokusanywa nje ya Mfumo wa DHIS2 kama vile GoT- HoMIS, eMR, VIMS-BID, CTC ziwe zinapatikana katika mfumo wa DHIS2 ili kuwezesha Sekta ya Afya kupata viashiria vya Kitaifa na kusisitiza uimarishwaji wa vitabu vya kukusanyia takwimu hizo.

"Tukiwa tunaendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki lakini pia hakikisheni vitabu vyote vya kukusanyia takwimu vinajazwa kwa usahihi kwa kuwa takwimu sahihi zinasaidia kujua kazi zetu tulizokabidhiwa na majukumu kama tumeyafanya kwa usahihi." Alisema Dkt. Jingu

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu alisema Upatikanaji sahihi wa takwimu utawezesha uwepo na upatikanaji wa dawa kwa kipimo sahihi kulingana na uhitaji wa maeneo husika.

"Sekta ya Afya inaendelea kuwekeza katika upatikanaji wa huduma kwa Jamii ambapo elimu sahihi ya Kinga itakuwa inatolewa pamoja na utambuzi wa mapema wa magonjwa mbalimbali, hivyo takwimu sahihi na zinazotolewa kwa wakati ni nguzo ya mafanikio ya juhudi hizi." Alisema Prof. Nagu.

Nae Kaimu Mkurugenzi Ufuatiliaji na tathmini kutoka Wizara ya Afya, Claud J. Kumalija alisema malengo ya kikao ni kufanya tathmini ya hali ya sasa ya takwimu za Afya na kuazimia, kujadili bunifu mpya zitakazo lenga kuwezesha mifumo ya takwimu za Afya kusomana kupitia mfumo wa DHIS2 na kuwezesha takwimu kuwafikia wahitaji kwa njia rahisi ya simu za mikononi ili takwimu za Afya ziweze kutumika katika mipango na maamuzi ya Sekta ya Afya nchini.






# Epukeni vishawishi, chipsi ni chakula kama vyakula vingine - Waziri Ummy

**Na. Emmanuel Malegi,**
**Dodoma**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu aliwataka vijana wenye rika balehe (hasa wasichana) kuepuka vishawishi kama chipsi na vingine ili kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI.

Waziri Ummy ambae pia ni mbunge wa Jimbo la Tanga Mjini alisema hayo wakati akifunga kampeni ya Jikubali katika viwanja vya Usagala, Halmashauri ya Jiji la Tanga ikiwa ni tayari imeshazifikia Halmashauri 18 za Mikoa mbalimbali ikiwemo Dodoma.

“Wanangu, njia za kupata maambuzi ya VVU na UKIMWI zipo nyingi lakini epukeni vishawishi kama chipsi kwa kuwa chipsi ni chakula Kama vyakula vingine, tusikubali kudaganyika kwa vishawishi vyovyote vile.” alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alisema Serikali kupitia Wizara ya Afya imepanga kutokomeza VVU na UKIMWI ifikapo mwaka 2030 ambapo imelenga kuwa na Sifuri Tatu katika maeneo ya maambukizi mapya, vifo na unyanyapaa.

“Kampeni hii ya JIKUBALI itatusaidia kwa kiwango kikubwa kama nchi kufikia malengo makuu ya kutokomeza VVU na UKIMWI ifikapo mwaka 2030 ambapo tumelenga kuwa na sifuri tatu katika maeneo ya maambukizi mapya, vifo na unyanyapaa.” alisema Waziri Ummy

Waziri Ummy.ameongeza kuwa takwimu za utafiti wa viashiria vya UKIMWI nchini iliyofanyika mwaka 2016-2017 zinaonyesha hali ya maambukizi iko juu zaidi kwa vijana wa kike, ukilinganisha na wa kiume.

alisema, kwa vijana wenye umri kati ya miaka 10 hadi 14, asilimia 0.3 wa kike na asilimia 0.3 wa kiume wanaishi na maambukizi ya VVU, wenye umri kati ya miaka 15 hadi 19 wa kike ni asilimia 1.0 na wakiume ni asilimia 0.4 na kwa wale wenye umri kati ya miaka 20 hadi 24 wa kike ni asilimia 3.4 wa kiume ni asilimia 0.9.

“Hali hii ya maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa vijana inatuamsha kama Serikali kubuni afua mahususi za kinga zinazolenga kundi hili la vijana rika balehe (hasa wa kike), ikiwemo utoaji wa elimu ya VVU na UKIMWI kwa njia ya Elimu Burudani (edutainment) kupitia watu maarufu na wasanii wenye wasifu wa kushawishi ili kuleta mabadiliko chanya ya tabia hatarishi kwa maambukizi ya VVU miongoni mwa vijana rika balehe mashuleni, ambayo imetuonesha mafanikio makubwa sana”. alisema Waziri Ummy

# NHIF yapewa miezi 3 kuboresha mifumo ya Tehama

**Na. Majid Abdulkarim, Dodoma**

Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel aliitaka Menejimenti ya Mfuko wa Bima ya Afya katika kipindi cha miezi mitatu ihakikishe inaboresha mifumo ya Tehama itakayoweza kuondoa usumbufu na pia kudhibiti udanganyifu pasipo kuwa kero kwa wanufaika wa Mfuko.

Dkt. Mollel alitoa agizo hilo wakati akijibu swali Namba 149 kwa Niaba ya Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu, kutoka kwa Mbunge wa Geita Mjini, Mhe. Constantine John Kanyasu aliyeuliza kwa nini NHIF inazuia matibabu ya baadhi ya wagonjwa wenye Bima za Afya wakiwa Hospitali.

“Ni kweli kulikuwa na zoezi la uhakiki wa uhalali wa wanufaika wa mfuko wa bima ya Afya, zoezi hilo lilileta usumbufu ambao ungeweza kuzuilika kama wahakiki hao wangetumika wataalamu wenye miiko ya taaluma ya tiba”, alieleza Dkt. Mollel

Dkt. Mollel alisema Serikali ilipopata malalamiko hayo ilifuatilia mara moja na kufanya maboresho ambayo yaliyoondoa usumbufu kwa wateja na wateja kuendelea kupata Huduma kwa ufasaha.

Kwa upande wake Mbunge wa Geita Mjini, Mhe. Constantine John Kanyasu, amempongeza na kufurahishwa Naibu Waziri wa Afya Dkt Godwin Mollel kwa kujibu maswali kwa ukweli

ISO 9001:2015 CERTIFIED





# Watu zaidi ya laki tatu kupata kingatiba dhidi ya Matende na Mabusha Kinondoni

**Na Said Nyaoza**
**Dar Es Salaam**

Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele (NTD) kwa kushirikiana na wadau wa Research Triangle Institute (RTI) inatarajia kufanya zoezi la umezeshaji kingatiba dhidi ya Ugonjwa wa Matende na Mabusha au Ngirimaji kuanzia Tarehe 6 mpaka 12 mwezi Disemba mwaka 2023 katika Manispaa ya Kinondoni Mkoani Dar es Salaam kwa Wananchi Takriban 333,584 wenye umri wa kuanzia miaka mitano na kuendelea.

Akifungua mafunzo kwa Waandishi wa habari kuhusu Ugonjwa Wa Matende na Mabusha ili waweze kushiriki katika kuelimisha na kuhamasisha jamii iweze kushiriki kwenye zoezi la umezeshaji wa kingatiba hizo Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule alisema Wilaya ya Kinondoni itahakikisha inaendelea kuweka jitihada za kutosha katika kutokomeza magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele (Mabusha na Matende).

"Ni wajibu wetu kuhakikisha tunaongeza uelewa kwenye masuala ya magonjwa yasiyokuwa hayapewi kipaumbele (NTD) lakini pia tunakuwa sehemu ya kutoa elimu na hamasa na kufuatilia katika ngazi za Jamii kila tunapopata nafasi ya kuzungumza na wananchi ili wawe sehemu ya kupata chanjo kama ambayo imeelekezwa". Alisema Mhe. Mtambule .

Mhe. Mtambule alisema magonjwa haya yanaweza kuzuilika kwa kupata kingatiba ama kupata tiba kwa ambao wanaugua na kwa kufanya hivyo tunaweza kuyaondoa kabisa kwenye jamii yetu.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Kinondoni Dkt. Samwel Laizer alisema kingatiba hizo zinatarajiwa kutolewa katika kata 10 za wilaya hiyo ambazo ni Kigogo, Mzimuni, Magomeni, Ndugumbi, Tandale, Kijitonyama, Kinondoni, Hananasif, Mwananyamala na Makumbusho kwa watu wote kuanzia miaka mitano na kuendelea.

"Tumepanga kugawa kingatiba hii nyumba kwa nyumba katika jamii husika, na katika maeneo yote ya mikusanyiko ikiwemo Mashuleni, nyumba za ibada, Masoko, Stendi za Mabasi na Vituo vya kutolea huduma za Afya, katika kata husika lengo ni kuhakikisha kwamba walengwa wote wanapata dawa ili tuweze kuyatokomeza Magonjwa hayo". Alisema.

"Tunagawa kingatiba hizi kwa sababu tukimeza wote katika jamii tunapunguza maambukizi kwa wakati wote na kuongeza kinga kwa wagonjwa pamoja na kupunguza ongezeko la ugonjwa wa matende na mabusha". Alisema.

Nae Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Kinondoni Mhe. Songoro Mnyonge alitoa wito kwa watu wote wenye dalili za ugonjwa wa matende na mabusha wajitokeze kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya ili waweze kutibiwa maana magonjwa hayo yanatibika na kupona kabisa.

# TMDA kupewa jukumu la usimamizi wa Maduka ya Dawa

**Na. Emmanuel Malegi, Dodoma**

Usugu wa vimelea dhidi ya dawa mwilini (Antimicrobial resistance AMR) ni tishio kubwa la afya kwa jamii ya Watanzania hivyo Serikali imeweka mikakati madhubuti ili kukabiliana na tatizo hilo kwa kuimarisha udhibiti kwa kuondoa usimamizi wa maduka ya Dawa kutoka Baraza la Famasi na kupeleka majukumu haya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)

Waziri Ummy alibainisha hayo kwenye ukurasa wake wa mtandao X wakati akijibu hoja ya Frank Arabi alipohoji kuhusu matumizi sahihi ya dawa za antibiotiki.

Waziri Ummy alisema kumekuwepo na matumizi yasiyo sahihi ya dawa nchini na hivyo kufanya dawa nyingi za Antibiotiki hivyo kuwa na ufanisi mdogo katika kutibu magonjwa.

“Pamoja na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya dawa za Antibiotiki, tatizo hii kwa kiasi kikubwa linachochewa na baadhi ya wataalam wetu kwenda kinyume na kanuni na miongozo ya taaluma”. alisema Waziri Ummy.

Waziri Ummy aliwataka wahudumu wa Afya hasa Madaktari na Wafamasia kusimamia jukumu hilo ili watanzania wapate uelewa juu ya matumizi sahihi ya dawa.





# Fanyeni kazi kwa uadilifu na ufanisi ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

**Na. Shaban Juma,**
**Tanga.**

Naibu Katibu Mkuu wizara ya Afya Dkt Grace Magembe aliwataka watumishi wa afya nchini kuwajibika kwa kufanya kazi kwa ufanisi na uwadilifu ili ili kutimiza malengo ya Serikali ya awamu ya sita ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

Dkt. Magembe alitoa kauli hiyo wakati wa kikao chake na watumishi wa afya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Bombo (Tanga) ambapo alisema watumishi wanatakiwa wajitume katika kuwahudumia wananchi.

“Wapo baadhi ya watumishi wanaofanya kazi kwa mazoea na wamehusika kwenye vitendo ambavyo ni kinyume na maadili, tutawachukulia hatua kali kwa sababu wanaharibu taswira ya sekta ya Afya”. alisema Dkt. Magembe

Aidha Dkt. Magembe alikemea vitendo vya utoroshwaji wa wagonjwa na kuwasababishia wananchi gharama zisizo za lazima huku akisisitiza hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa kila atakaebainika.

“Zipo taarifa za baadhi yenu kutorosha wagonjwa kupeleka kwenye hospitali za nje badala ya kuendelea kupata huduma kwenye hospitali za umma na hivyo kuwasababishia wananchi usumbufu na gharama zisizo za lazima, tutashuhulika na wewe". alisema Dkt Magembe

Hata hivyo Dkt. Magembe aliwasisitizia watumishi hao kufanya kazi kwa ushirikiano na kila mmoja awe tayari kujifunza mazuri kutoka kwa mwenzie ili wote wafanye kazi iliyo nzuri.

"Ni imani yangu hatutasikia wala kuona uzembe wa aina yoyote, bali mtabadilika na kufanya kazi zenu kwa bidii, ubunifu na uweledi mkubwa ili kutimiza malengo ya Serikali ya awamu ya sita ya kutoa huduma bora kwa wananchi wake". Alisisitiza Dkt. Magembe

# Kliniki tembezi kuibua wagonjwa wa TB, UKIMWI na Malaria




**Na Cletus Sanga, Dodoma**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema magari ya Kliniki Tembezi (Mobile Clinic) yakatumike katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB) hususani kuibua wagonjwa wapya, UKIMWI pamoja na Malaria.

Waziri Ummy alisema hayo wakati wa makabidhiano ya magari hayo ya Kliniki Tembezi yenye thamani ya Mil. 618,477,000/= yaliyofanyika Mkoani Dodoma.

"Karibu 35% ya wagonjwa wa Kifua Kikuu bado tunao katika majumba yetu, ofisi zetu, vijiji vyetu na mitaani kwetu, Kwahiyo naamini kabisa magari haya yatatumika katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa TB kwa kuibua wagonjwa wapya, mapambano dhidi ya Malaria na UKIMWI". alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alisema magari hayo (Mobile Clinic) yatakuwa yanatoa huduma za Afya za kisasa katika jamii ambayo ipo mbali na huduma za Afya pamoja na kutembea katika masoko na stendi za magari kutoa huduma za upimaji.

"Magari haya pia yatumike kutoa huduma za chanjo kwa watoto ambao wanapaswa kupata chanjo, pia yakatumike kwenye mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza na mtu akikutwa na changamoto basi aambiwe aende kwenye kituo cha kutoa huduma za Afya kwa matibabu zaidi". alisema Waziri Ummy

Aidha Waziri Ummy alisema, Tanzania ina changamoto ya magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo Kisukari ambapo katika kila watu 100 wenye umri wa miaka 15 na kuendelea watu 9 wana ugonjwa wa Kisukari, changamoto ya watu wenye Shinikizo la Juu la Damu ambao ni 25% na hawajui.

"Nitoe shukrani nyingi sana kwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kujali Afya za Watanzania kwa kuendeleza mashirikiano na Mataifa mbalimbali na kuja kuwekeza nchini hasa katika Sekta ya Afya". alisema Waziri Ummy

Mwisho, Waziri Ummy alishukuru uongozi wa Aga Khan - Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) kwa kuwekeza kwenye Sekta ya Afya na kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Rais Samia katika kuboresha mifumo ya utoaji wa huduma za Afya nchini.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu OR - TAMISEMI Dkt. Wilson Mahera alisema magari hayo (Kliniki Tembezi) yatakwenda kusaidia upatikanaji wa huduma za Afya kwa haraka katika Jamii ambazo zipo mbali na vituo vya Afya.
Pia, alisema watasimamia na kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu ikiwemo ya usimamizi mzuri wa karibu pamoja na maendeleo ya mradi huo ikiwa ni pamoja na shughuli zote zitakazotekelezwa na magari hayo ya kliniki tembezi.

# Apollo yaanza tathmini ujenzi wa Hospitali Dar es salaam

**Na Said Nyaoza**
**Dar Es Salaam**

Uongozi wa Kituo cha Umahiri na Ubobezi wa Kimatibabu 'Apollo Hospitali' kilichopo nchini India umeanza kutathmini eneo itakapojenga Hospitali jijini Dar es Salaam ambapo uwekezaji huo utakaoleta chachu katika Sekta ya Afya.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu wakati wa mazungumzo na Rais wa Apollo Group Hospitals, Dkt. K Hari Prasad kilichofanyika Jijini Dar es Salaam.

Alisema, majadiliano hayo yamefuatia kati ya Rais Samia na uongozi wa Hospitali hiyo yaliyofanyika Oktoba 11 mwaka huu ambapo hadi sasa ni siku 27 tu zimepita tangu majadiliano hayo yafanyike.

Aidha, Dkt. Jingu alisema ndani ya miaka mitatu Hospitali hii itakuwa imeshajengwa na inafanya kazi, tuna kila sababu ya kumshukukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona jambo hili ni muhimu ambapo uwekezaji huo utazidi kuboresha huduma za Afya.

Wakati akiendelea kuelezea umuhimu wa Hospitali hiyo Dkt. Jingu alisema kuwa hatua hiyo ni katika kuhakikisha Tanzania inakua na kituo cha umahiri ukanda wa kusini mwa Africa lakini pia ukanda wa Afrika Mashariki ambapo Tanzania imewekeza katika kuboresha huduma za Afya hivyo kituo hiko cha umahiri kitaongeza utalii wa matibabu na watu wote watakuja kupata huduma za Afya nchini". alisema Dkt. Jingu

Kwa upande wake Rais wa Apollo Group Hospitals, Dkt. K Hari Prasad wakati akizungumzia mchakato unaoendelea baada ya kikao cha siku tatu kati ya hospitali hiyo na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya alisema wamekuja Tanzania kuanzisha kituo cha matibabu bobezi ili kuongeza ubora wa huduma za Afya nchini.

"Sisi tunaziba pengo lililopo na hatuji kwa sababu ya mashindano na watoa huduma wengine, tunaamini katika hili na ujio wa bima ya afya kwa wote pia utasaidia watu kupata huduma bora zaidi Tanzania na Baraza la Afrika". alisema Dkt. Prasad

alisema, katika mazungumzo yao na Rais Dkt. Samia ambapo amesisitiza namna watakavyosaidia kuleta huduma za kibingwa nchini ikiwemo matibabu kwa watoto wenye matatizo ya moyo na hasa yale magonjwa ambayo bado Watanzania wanafuata huduma hizo nchini India.

Nae, Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu alisema wamekaa na uongozi wa Apollo kwa siku tatu na kufanya makubaliano kadhaa ikiwemo eneo ambalo Hospitali hiyo itajengwa





# Watendaji 7 MSD waondolewa kwa kukiuka sheria ya manunuzi ya vifaa tiba ya Tsh Bilioni 3.4

**Na. Englibert Kayombo**
**Dodoma**

Watendaji saba wa Bohari ya Dawa (MSD) waliondolewa kazini kufuatia ukiukwaji wa sheria ya ununuzi wa vifaa tiba vyenye thamani ya Tsh billion 3.4 kutoka kampuni ya Misri ya Al Andasia.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu wakati akijibu hoja zilizoibuliwa na Kamati za PAC, PIC na LAAC katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali (CAG) ya mwaka 2021/2022 Bungeni Jijini Dodoma.

“Serikali ilichukua hatua za kiutawala ambapo ilimuondoa Mtendaji Mkuu wa Bohari ya Dawa mwezi Aprili 2022 pamoja na Wakurugenzi wengine sita akiwemo wa Utawala, Fedha na mipango, Ununuzi, Usambazaji wa huduma za kanda, Meneja wa Sheria na Mkaguzi Mkuu wa ndani wa MSD. Aidha ulifanyika ukaguzi maalum wa eneo la ununuzi na kubadilisha watumishi 24 kabla ya CAG kati ya Juni - Desemba 2022” alisema Waziri Ummy Mwalimu.

alisema utendaji wa sasa wa Bohari ya Dawa umeimarika baada ya kuongeza thamani ya bidhaa zilizosambazwa kutoka Bilioni 315 mwaka 2021/2022 hadi kufikia Shilingi Bilioni 373 mwaka 2022/2023 ambapo thamani hii haihusishi bidhaa za miradi msonge.

“Katika robo ya mwaka kuanzia Julai - Septemba 2023 thamani ya bidhaa zilizosambazwa ni bilioni 113 ukilinganisha na bilioni 77 za Robo ya Julai - September 2022 sawa na ongezeko la 45%” alisema Waziri Ummy.

Akijibu kuhusu hoja ya serikali kutokulipa madeni ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ya TSH bilioni 228, Waziri Ummy alisema kuwa Serikali imekubali kulipa Shilingi Bilioni 228 za NHIF ambazo ni deni la Wizara ya Mambo ya Ndani Shilingi Bilioni 45.4, Taasisi ya Mifupa (MOI) Shilingi Bilioni 18.2, NIDA sh. bilioni 17.3 na Hospitali ya Benjamin Mkapa Shilingi Bilioni 129.

Waziri Ummy alisema kuwa madeni hayo yatalipwa ili kulinda uhai na uendelevu wa Mfuko. Mhe. Ummy aliyasema haya wakati akijibu hoja za ripoti ya CAG ya 2021/2022.

"Kila senti inayotolewa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenda kwenye Sekta ya Afya tutaisimamia, na nitume salamu kwa Watendaji wote wa MSD na wengine wa Sekta ya Afya watakaofanya ubadhirifu hatutawavumilia, tutachukua hatua mara moja ili kulinda fedha za Serikali" alisema Waziri Ummy.



# Watu zaidi ya laki tatu kupata kingatiba dhidi ya Matende na Mabusha Kinondoni

**Na Emmanuel Malegi**
**Dodoma**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu aliliagiza Baraza la Madaktari Tanganyika kuendelea kuendesha mitihani miwili ya kabla na baada ya Utarajali kwa Madaktari wote nchini wanaomaliza vyuo na kuuanza mafunzo kwa vitendo.

Waziri Ummy alisema hayo jijini Dodoma wakati akipokea taarifa ya matokeo ya uchunguzi wa kamati huru kuhusu ufaulu wa mitihani ya watarajali inayoendeshwa na Baraza la Madaktari Tanganyika kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati Prof. Mohammed Kambi.

Waziri Ummy alisema Daktari yeyote aliyemaliza masomo yake katika vyuo vya udaktari ndani na nje ya nchi ili apate leseni ya Udaktari ni lazima afanye mtihani wa kabla ya utarajali na baada ya kukamilisha kipindi cha utarajali.

Aidha, Waziri Ummy alilitaka Baraza la Madaktari Tanganyika kuzingatia miongozo ya alama za ufaulu kama ilivyoelekezwa ili kusimamia taaluma ya udaktari na endapo daktari atashindwa kufikia alama zilizopendekezwa kwenye muongozo itabidi arudie mitihani.

Waziri Ummy aliliagiza Baraza la Madaktari Tanganyika kutoruhusu daktari aliyefeli Mtihani wa utarajali kuendelea na mafunzo kwa vitendo badala yake itamlazimu arudie mtihani huo mpaka afaulu ndipo aendelee na mafunzo kwa vitendo (Internship).

Kwa upande mwingine Waziri Ummy alisema Wizara ya Afya itaendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu pamoja na na vyuo na taasisi za Ithibati ili kuboresha mafunzo kwa upande wa Madaktari wakiwa vyuoni.

Waziri alisema kuwa Wizara ya Afya itaendelea kutimiza jukumu la kumlinda Mwananchi kwa kuhakikisha anapata huduma bora kutoka kwa wanataaluma wa Afya waliothibitishwa na Mabaraza ya kitaaluma kuwa ulinganifu na ubora unaotakiwa utakaowezesha kutoa huduma za afya bora kwa wananchi.

Akiwasilisha mapendekezo ya Kamati, Mwenyekiti wa Kamati hiyo prof. Mohammed Kambi alisema Kamati imependekeza mitihani ya utarajali kuendelea kufanyika licha ya madaktari kulalamikia ufaulu mdogo huku akilitaka Baraza la Madaktari Tanganyika kutoa alama za ufaulu kwa madaktari waliofanya mitihani hiyo.

# Tanzania kuwa kitovu cha tiba utalii

**Na Said Nyaoza**
**Dar Es Salaam**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema kuwa Tanzania inakwenda kuwa kitovu cha Tiba Utalii kwa kutoa huduma za Afya kwa wagonjwa maalumu wa ndani na nje ya nje.

Waziri Ummy alisema hayo Novemba 28, 2023 baada ya kufungua mradi wa kliniki mpya ya wagonjwa maalum na wa kimataifa iliyopo katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI) itakayotoa huduma za kliniki kwa wagonjwa wa ndani na nje ya nchi.

"Haya tutakayoyashuhudia leo ni matokeo ya uwekezaji mkubwa ambao Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amefanya katika Sekta ya Afya lakini pia niwapongeze Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) chini ya Prof. Abel Makubi na Mwenyekiti wa Bodi Prof. Charles Mkony kwa kazi nzuri na kubwa ya kuokoa maisha ya Watanzania". Alisema Waziri Ummy.

Waziri Ummy aliwaomba Watanzania wenye uhitaji wa tiba kwa haraka (kliniki ya wagonjwa maalum na Wakimataifa) ikiwa ni mtumishi au mfanyabiashara waende MOI ambapo ndani ya masaa mawili unamaliza kila kitu na kuendelea na shughuli zako.

Aidha, Waziri Ummy aliitaka Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI) iendeshe kliniki hiyo mpya ya wagonjwa maalum na wa kimataifa kwa ubia na wawekezaji wengine ili kuboresha zaidi huduma zitolewazo.

"Ni jambo zuri sana mmelianzisha lakini tusije kukwama njiani hivyo tushirikiane na wadau wengine ili huduma hii iendelee na ni matarajio yangu kwamba kliniki hii mpya ya wagonjwa maalumu na wagonjwa wa Kimataifa itakuwa kliniki ya mfano ambayo itakua kivutio kikubwa kwa wagonjwa kutoka katika Mataifa mbalimbali". Alisema Waziri Ummy.

Alisema, Kutokana na uwekezaji mkubwa katika miundombinu vifaa tiba na wataalamu, Taasisi ya MOI imefanikiwa kupunguza rufaa za wagonjuwa kwenda nje ya nchi ambapo hivi sasa 99% ya huduma za mifupa zinapatikana hapa nchini na 97% ya huduma za kibingwa za Ubongo, Mgongo na Mishipa ya fahamu zinapatikana hapa chini.

Mwisho, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusikiliza kilio cha Watanzania na kuboreha huduma za Afya ikiwemo kutoa fedha kwaajili ya majengo, vifaa na vifaa tiba na Sasa tunakwenda kuwa kitovu cha Tiba Utalii.






# Fanyeni tafiti ili kuboresha huduma za Maabara

**Na Shaban Juma**
**Dodoma**

Wahitimu wa mafunzo ya uongozi wa maabara chini ya programu ya Global laboratory Leadership Program (GLLP) wametakiwa kufanya tafiti katika huduma za uchunguzi wa magonjwa katika sehemu ya usimamizi wa huduma za maabara ili kudumisha huduma za uhakika katika maabara Nchini.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa Huduma za Dharura na maafa Wizara ya Afya Dkt. Elias Kwesi wakati akimuwakilisha Katibu mkuu wa Wizara ya afya Dkt. John Jingu katika mahafali ya mafunzo ya uongozi wa maabara kupitia programu ya Global Laboratory Leadership Program iliyofanyika Novemba 29, 2023 jijini Dodoma.

Dkt. Kwesi alisema kupitia tafiti ambazo zitafanywa na wahitimu hao itasaidia katika kuchunguza na kugundua namna ya kuboresha huduma za maabara katika hospitali, vituo vya afya na zahanati.

"Nendeni mkafanye tafiti, tafiti hizi zitasaidia katika kuboresha huduma za maabara hasa katika uchunguzi wa magonjwa na kuboresha huduma zenyewe". Alisema Dkt. Elias.

Aidha Dkt. Kwesi alisema ili kuweza kufanikiwa ni vyema kwa wahitimu wakazingatia na kuyafanyia kazi mafunzo waliopata ili kudumisha ubora Nyanja za maabara kwa kutoa huduma nzuri.

Hata hivyo Dkt. Kwesi aliongeza kuwa eneo la maabara ni eneo la heshima, hivyo ukiingia maabara unatakiwa uwe na heshima kwai ni sehemu nyeti kwa ajili ya uchunguzi na utoaji wa huduma.





# Dkt. Jingu ashiriki uzinduzi wa mkutano wa SADC wa Mawaziri wa Afya akimuwakilisha Waziri Ummy.

**Luanda, Angola**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu amemuwakilisha Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu katika mkutano wa Jumuiya ya SADC wa Mawaziri wa Afya na Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya UKIMWI unaoendelea Luanda Nchini Angola kuanzia Novemba 25 - 29,2023.

Awali Dkt. Jingu ameshiriki Uzinduzi wa Mkutano huo ulifanyika kwa njia ya matembezi na maandamano kwa washiriki kubeba mabango yenye jumbe mbalimbali zenye Kaulimbiu isemayo "Community led" uzinduzi ambao ni sehemu ya nchi za Jumuiya ya SADC kushirikiana na nchi mwenyeji kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI miongoni mwa nchi wanachama.



Katika Mkutano huo, Mawaziri na wawakilishi wao wanatarajiwa kujadili masuala ya afya yenye lengo la kuchangia katika kufanikisha uboreshaji wa hali ya maisha ya wananchi katika nchi wanachama, kuchunguza hali ya utekelezaji wa maamuzi ya vikao vyao vya pamoja vya awali na kupitia hali ya afya katika ukanda wa SADC.

Mawaziri wa afya pia watahudhuria maadhimisho ya Siku ya Malaria ya SADC Luanda - Angola tarehe 29 Novemba 2023.

# Rais Dkt. Samia achagiza mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya VVU.

**Na Cletus Sanga**
**Morogoro**

Tanzania chini ya Uongozi wa Dkt Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Afya, imekuwa kati ya nchi zinazoonyesha mafanikio katika kupambana na maambukizi mapya ya VVU kwa kiwango kikubwa.

Kauli hiyo ilitolewa na mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Mahenge, ambaye ni Afisa Tawala wa wilaya Mahenge, Huruka Rajabu wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Jikubali katika viwanja vya Mapinduzi wilayani Mahenge katika Mji wa Ulanga, Novemba 1, 2023.

alisema kuwa wilaya hiyo imeongeza maeneo ya kutolea huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU na huduma rafiki kwa Vijana ikiwa ni kuunga Mkono jitihada za Kupambana na Ugonjwa huo.

"Serikali imeendelea kuimarisha mapambano kwa kutenga fedha za Ujenzi wa Vituo vya kutolea Huduma za Afya pia huduma ya upimaji zinapatikana hata kwenye maeneo yenye viashiria vya maambukizi ya VVU kama vile kumbi za starehe, Nyumba za wageni, kwenye mabwawa na machimbo ya madini" alisema Huruka Rajabu

Aliongeza kuwa moja ya mambo ambayo pia serikali wilayani hapo inafanya na kuongeza idadi ya watu wanaotambua hali zao na upatikananji wa huduma rafiki

"Nitoe rai kwa vijana wote wajitokeze kwa wingi katika huduma za upimaji wa VVU kwa hiari ili wale watakaogundulika kuwa wana maambukizi ya VVU waweze kuanza dawa za ARV mapema ili watimize ndoto zao" alitoa wito Huruka

Kwa upande wake Mhandisi wa wilaya hiyo Amiri Mbuye akizungumza kwa niaba Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Mahenge, alisema kupitishwa kwa sheria ya upimaji VVU ambayo imepunguza umri wa vijana wanaotakiwa kupima VVU kwa ridhaa ya mzazi au mlezi kutoka miaka 18 hadi 15, na pia kuruhusu huduma za upimaji binafsi wa VVU, itasaidia kuwawezesha Vijana Kutambua hali zao za Maambukizi na Kuchukua Hatua stahiki za kujilinda.



# Hakikisheni watoto wachanga hawapati shida watumiapo kadi za wazazi wao.

**Na. Majid Abdulkarim, Dodoma**

Naibu Waziri wa Afya, Dkt.Godwin Mollel aliwataka watendaji wa mfuko wa bima ya afya na vituo vyote vya huduma za afya nchini kuhakikisha watoto na wazazi hawapati shida iwapo mama atakuwa na kadi yake inayoonyesha ushahidi wote kuhusu mtoto husika na ni mtoto wangapi kwenye familia.

Dkt. Mollel alitoa agizo hilo Jijini Dodoma katika Mkutano wa Bunge wa 13 Kikao cha Nne wakati akijibu swali kwa niaba ya Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu, swali Namba. 61 kutoka kwa Mbunge wa Viti Maalumu, Mhe. Martha Nehemia Gwau aliyeuliza Je, Serikali haioni kuna haja ya Watoto wachanga kutumia Bima za Afya za Mama zao

Dkt. Mollel alisema kuwa Serikali chini ya Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ilishatoa maelekezo kwa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuhakikisha watoto wachanga wenye uhitaji wa huduma wanapata huduma za afya bila kikwazo chochote.

Vile vile Dkt. Mollel aliongeza kuwa watoto wanaozaliwa katika hospitali na vituo vya kutolea Huduma za afya nchini ambao wazazi wao wana bima za afya watibiwe kwa kutumia bima za wazazi wao.

"Niwaase wazazi na viongozi wa hospitali husika kukomesha kabisa matukio ya kughushi nyaraka ambazo pia ndio zinapelekea kuwepo kwa usumbufu wakati mwingine", alitoa wito Dkt. Mollel.







# Waganga wa kienyeji sio suluhu ya matibabu ya Kifua Kikuu

**Na. Abdulwaheed Madenge, Kilimanjaro**

Kukosekana kwa elimu ya Wataalam wa afya waliobobea katika kuwahudumia wagonjwa kila siku, imewafanya baadhi ya Wananchi kwenda kwa waganga wa kienyeji kupata tiba za ugonjwa wa Kifua Kikuu wakidhani kuwa wamerogwa.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Hospitali Maalumu ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto Dkt. Leonard Subi wakati akizungumza kwenye ufunguzi wa zoezi la upimaji wa ugonjwa wa Kifua Kikuu, Virusi vya Ukimwi, shinikizo la damu zoezi lililofanyika katika kitongoji cha Orengetwa Kata ya Sanya Juu Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro.

Dkt. Subi alisema kukosekana kwa elimu hiyo, imesababisha baadhi ya Wananchi kukimbilia kwa waganga wa kienyeji wakidhani wamerogwa kabla hawajagundua kama wanaumwa Kifua Kikuu.

"Licha ya serikali kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi kwenda kwenye vituo vya afya kupima afya zao pindi wanapoona dalili za Kifua Kikuu wako baadhi ya wananchi huenda kwa waganga wa kienyeji kupata tiba hiyo jambo ambalo limetusukuma sisi kutoka katika kituo chetu cha kazi kwenda vijijini kwa ajili ya kutoa elimu hii". alisema Dkt. Subi.

Dkt. Subi alisema kuwa takwimu zinaonyesha kuwa watu zaidi ya milioni 10.4 wanaugua Kifua Kikuu kila mwaka na kati yao watu milioni 1.6 wanafariki dunia kutokana na ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB) na nchi ya Tanzania inatajwa kuwa ni miongoni mwa nchi duniani yenye maambukizi ya Kifua Kikuu ambayo yako juu.

"Pamoja na jitihada za ugonjwa wa Kifua Kikuu kupungua , bado kuna wagonjwa wa Kifua Kikuu ambao wako kwenye jamii na wale wanaowagundua ni asilimia 65 tu, huku asilimia 35 wako kwenye jamii na hao ndiyo tunawatafuta ili waweze kupatikana kwa lengo la kuwaweka kwenye matibabu". alisema.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Siha Dkt. Paschal Mbota alisema Wilaya ya Siha ina vituo vya kutolea huduma za afya 27 na kati ya hivyo vituo 12 vinauwezo wa kupima ugonjwa wa Kifua Kikuu

Aidha, Dkt. Mbota alisema kadri ambavyo wamekuwa wakifanya zoezi la upimaji wa ugonjwa wa Kifua Kikuu wamekuwa wakiwaibua wagonjwa wengi wa Kifua Kikuu na kuwapatia matibabu jambo ambalo limesaidia kupunguza kasi ya kuenea kwa ugonjwa huo.

# Dola milioni 250 kuboresha huduma za afya ya uzazi mama na mtoto.




**Na. Englibert Kayombo**
**Dodoma**

Katika kuendeleza juhudi za uboreshaji huduma za Afya ya Uzazi Mama na Mtoto, Serikali kupitia Wizara ya Afya inatekeleza programu ya uboreshaji huduma hizo ujulikanao kwa jina la 'Tanzania Martenal and Child Health Investment Program (TMCHIP)' kwa miaka Mitano ukiwa na thamani ya zaidi ya Dola Milioni 250.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alipokutana na Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Dunia Dkt. Juan Pablo Urine kwenye kikao kilicholenga kujadili uboreshaji wa huduma za Afya nchini.
"Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza program hii ya miaka Mitano kuanzia Januari 2023 hadi Disemba 2027, Programu hii inalenga kuboresha ubora wa huduma za Afya ya uzazi, mama na mtoto nchini". alisema Waziri Ummy

Waziri Ummy alisema kuwa kupitia programu hiyo, Serikali itaboresha vyumba/vituo 15 vya uangalizi wa Watoto njiti (NICU) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, kuboresha NICU 10 katika vyuo vya Afya na kuboresha Vituo vya ukusanyaji wa Damu Salam Sita.

"Tunatarajia kutoa mafunzo ya kitaalam kwa watoa huduma zaidi ya 10,000 pamoja na kutoa mafunzo elekezi kazini kwa wataalam zaidi ya 8,000 nchi nzima ili waweze kutoa huduma bora za afya ya uzazi mama na mtoto". alisema Waziri Ummy

Waziri Ummy alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea na mageuzi makubwa ya utoaji wa huduma za afya nchini kulingana na Mpango Mkakati wa tano wa Sekta ya Afya na Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano wa Tanzania.

Aidha, Waziri Ummy alisema kuwa jitihada zinahitajika zaidi na ushiriki wa wadau katika kuboresha zaidi huduma za Afya nchini na kuomba ushirikiano wa Benki ya Dunia katika eneo la uimarishaji wa huduma kutoka kwa watoa huduma za Afya ngazi ya jamii, ugharamiaji wa Bima ya Afya kwa Wote pamoja na kuweka mifumo imara ya huduma za dharura na udhibiti wa majanga.

Kwa upande wake Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Dunia Dkt. Juan Pablo Uribe aliipongeza Tanzania kupitia Wizara ya Afya kwa kuwa na mfumo wa kupeleka wagonjwa haraka kwa kutumia magari ya dharura (M-Mama).

# MSD mlipa kodi bora kwa mwaka 2023 nchini

**Na. Shaban Juma**
**Dodoma**

Bohari ya Dawa (MSD), imetwaa tuzo ya Mlipa kodi Bora kwa mwaka 2023 ya Mamlaka ya Kodi Tanzania.

Tuzo hizo zilitolewa katika hafla maalum ya wiki ya Mlipakodi zilizofanyika katika Ukumbi wa Mlimani City jijiini Dar es Salaam ambako Bohari hiyo imeibuka mshindi wa kwanza katika kipengele cha walipakodi wa Kati kwa Mkoa wa Kikodi wa Temeke.

Akipokea tuzo hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai amesema ushindi huo una maana kubwa kwa Bohari hiyo na Watanzania.
Amesema MSD ambayo ni moja ya Taasisi za kimkakati za Serikali inayohusika na kuzalisha, kununua, kutunza na kusambaza bidhaa za afya kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali nchini inafuata taratibu, sheria na miongozose ikiwa ni pamoja na kulipa kodi stahiki

"Maendeleo yoyote ya nchi yanategemea kodi zinazolipwa hivyo ni vyema kila mlipa kodi akalipa kodi stahiki ili kuwezesha muendelezo wa biashara na kuimarisha maendeleo kwa mustakali wa ustawi wa jamii, " ameongeza Tukai katika hafla hiyo ambako mgeni Rasmi alikuwa Naibu Waziri Mkuu, Dk Dotto Biteko.


Kwa mujibu wa Mkurugenzi Tukai, MSD sasa iko katika mkakati wa kujiendesha kibiashara hivyo hatua ya kulipa kodi kwa utaratibu uliowekwa hadi kutambuliwa ni fursa ya kuaminika kwa wadau wetu katika huduma tunazotoa.

Awali Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi na Mawasiliano TRA, Richard Kayombo alisema vigezo vilivyotumika kupata washindi ni kulipa kiasi kikubwa cha kodi na hiari pamoja na kutunza kumbukumbu vizuri.



# JE WAJUA?

Kutembea angalau kwa dakika 30 kwa siku kutakusaidia



- Kupunguza uzito
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kupunguza Shinikizo la Juu la Damu
- Kupunguza hatari ya kupata Magonjwa Yasiyoambukiza




Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
**WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI NOVEMBA, 2023**